ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
3. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
4. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
5.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
6. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
7. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
8. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge

9. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
10. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
11. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
12.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
14. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
15. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
17. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
18. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
20. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
21. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
22. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
23. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
24. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
26. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
27. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
28. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
29. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
30. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
31. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
32. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
33. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
34. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani

35. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
36. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
37. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
39. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
40. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
42. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
43. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
44. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
45. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
46. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
47. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
48. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
49. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
50. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
51. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
52. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
53. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
54. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
55. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
56. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
57. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
58. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma - Jimbo la Chukwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
66. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake

71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tano – Tarehe 26 Mei, 2016

(Kikao Kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani kuhusu Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini (Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuweka mezani hotuba ya maoni ya Kamati ya Wenyeviti kuhusu Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 36

Ukosefu wa Jaji Mkaazi Pemba

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Kisiwa cha Pemba hakina Jaji Mkaazi na kusababisha kesi nyingi kuchelewa kutolewa hukumu wakati muafaka kutokana na baadhi ya Majaji wanaopangiwa kulazimika kusikiliza na kurudi Unguja na wengine kutokuenda kwa muda mrefu na kucheleweshe haki ya kisheria.

a) Kwanini serikali haipeleki Jaji Kisiwani Pemba ili wananchi wapate haki yao kisheria kwa wakati badala ya Majaji kwenda kwa msimu.
b) Kwa kuwa jambo hili limekuwa la muda mrefu na serikali inatoa ahadi bila ya kutekeleza je, haioni kitendo hicho ni kuwadanganya wananchi.

c) Kama serikali haina nyumba imeweza vipi kuwakodia baadhi ya Majaji nyumba ishindwe kwa Jaji mmoja.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 36 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, wizara inaona umuhimu wa kuwa na Jaji Mkaazi Pemba ingawa kwa sasa Mahakama ina uchache wa Majaji. Ili kutatua tatizo hili Mahakama imechukua hatua ya kupendekeza serikalini kuongeza idadi ya Majaji wa Mahakama Kuu kwa lengo la kuharakisha usikilizaji wa kesi. Hata hivyo, hatua ya kuongezwa kwa Majaji peke yake sio kigezo pekee cha kumpeleka Jaji Mkaazi Pemba, bali serikali inazingatia mambo mbali mbali, ikiwemo uwiano wa kesi kati ya Unguja na Pemba.

(b) Mhe. Spika, serikali imekuwa ikichukua hatua mbali mbali za kuhakikisha kwamba inatekeleza ahadi zake, ikiwemo kupeleka Jaji Kisiwani Pemba kwa lengo la kusikiliza kesi za Mahakama Kuu kadri mahitaji yanapojitokeza. Hatua hizo zimesaidia sana katika kupunguza mrundikano wa kesi katika Mahakama zetu za Pemba.

(c) Mhe. Spika, napenda kumjuulisha Mhe. Mwakilishi kwamba, ukiondoa Mhe. Jaji Mkuu, serikali haina utaratibu wa kuwakodia Majaji wengine nyumba. Majaji wetu wote wanaishi katika makaazi yao binafsi na serikali hutoa posho mbali mbali kwa Majaji hao, ikiwemo posho ya nyumba.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, kwa kuwa serikali imeahidi miaka mingi kupeleka Jaji Kisiwani Pemba, lakini ahadi hiyo mpaka hii leo haijatekelezwa.

(a) Ni lini ahadi hiyo itatekelezwa kwa vitendo na vile vile hivi sasa kuna kesi ngapi ambazo ziko katika Mahakama hiyo zinataka kusikilizwa.

b) Katika kupeleka Jaji kwa msimu Pemba hamuoni serikali inatumia gharama kubwa badala kuweka Jaji awepo pale ili kusikiliza kesi tena kwa

wakati. Na vile vile Mhe. Rais katika sherehe za Wanasheria aliahidi kuongeza Majaji wawili Kisiwani Pemba. Je, hivi sasa unakaribia nusu mwaka ahadi hiyo mmeifatilia vipi kwa vitendo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

(a) Mhe. Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba hivi sasa serikali imekuwa katika hatua za kuhakikisha kwamba Majaji Pemba wanapatikana. Hivyo, kwa kuwa tayari serikali imeshalijua hili na iko katika hatua za mwisho, nakuahidi *inshaallah* atakapopenda Mwenyezi Mungu wakati wowote kutoka sasa hivi Majaji hao watapelekwa Pemba. (*Makofi*)

b) Kuhusiana na suala la gharama kwa Majaji kuwatoa Unguja kwenda Pemba, hili suala kwa kiasi fulani ni kweli, lakini kama nilivyokwambia kwamba ili kuepuka hili hivi sasa serikali wakati wowote itapeleka hao Majaji Pemba ili kuhakikisha kwamba hizo gharama serikali haiingii.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii, napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri kwamba, sambamba na kupeleka Majaji kama imewezekana au haikuwezekana, lakini Pemba kuna matatizo ambayo kuwa mashahidi huku hutoka Tanzania Bara na kufika pale wametumia gharama zao na mashahidi wengine wanaokuja pale wanalazimika kutumia gharama kubwa kama vile ndege.

Je, Mhe. Naibu Waziri, anajipanga vipi katika kupata mafungu yake ya kila mwezi kuisaidia Pemba kupata pesa za mashahidi kama hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, ni kweli tatizo hilo limekuwa likijitokeza siku hadi siku lakini hivi sasa serikali imekusudia kuhakikisha kwamba suala hilo linaweza kuondolewa haraka iwezekanavyo. Kwa hivyo, Mhe. Mwakilishi, usiwe na wasi wasi tatizo hilo wakati wowote litaondoka na mashahidi hawatopata tabu katika kulipwa hicho ambacho wangekitumia.

Nam. 85

Wakulima Kupatiwa Huduma za Bure na Serikali

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:-

Tunaipongeza serikali kupitia Wizara yake ya Kilimo ambayo kwa muda mrefu imekuwa ikiwapatia wakulima pembejeo za kilimo ikiwemo mbegu, mbolea na madawa hatua ambayo imekuwa ikiwasaida sana wakulima wetu na kuwaongezea ari ya kushiriki katika shughuli za kilimo.

Je, lini serikali inafikiria kuwasaidia zaidi wananchi wake kwa kuwalimia bure (kuwavurugia) mashamba yao ili kuwapa motisha zaidi katika kazi zao za kilimo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 85 kabla ya kujibu naomba kutoa maelezo machache.

Mhe. Spika, wizara imejifunza kupitia Mradi wa Mpunga wa Kutegemea Mvua (*Rain fed Rice Development Project* (*RRDP*) uliokuwa na lengo la kuimarisha miundombinu ya kilimo kwa ajili ya kuongeza tija kwa eneo pamoja na kipato cha mkulima. Mradi huu ulipata mkopo wa fedha jumla ya dola za Kimarekani milioni 2.5 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*).

Mhe. Spika, mradi ulifanikiwa kununua matrekta 45 (Unguja 38 na Pemba 7) na kuwalimia wakulima mashamba bila ya kuchangia.

Mhe. Spika, mradi ulipata changamoto ya ushiriki na mchango mdogo wa wakulima katika utekelezaji wake kutokana na ile dhana kuwa huduma zote za mradi ni jukumu la serikali.

Mhe. Spika, baadhi ya wakulima waliyaacha mashamba hayo bila ya kuyapanda, jambo ambalo lilipunguza ufanisi wa utekelezaji wa mradi huo. Mhe. Spika, hivyo wizara inaandaa utaratibu wa kuwatambua wakulima ambao wanatumia fursa vyema zinazotolewa na serikali na wale ambao wanapuuza lakini wanayo mashamba yatalimwa na kupewa wakulima wenye shida ya ardhi.

Mhe. Suleiman Sarahani Said: Mhe. Spika, nina swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Kwa kuwa serikali inajitahidi kuwasaidia wananchi wake kwa upande wa ukulima, katika bonde la Tibirizi ile sehemu kubwa imeingia maji ya chumvi na wakulima hawana sehemu ya kulima kwa kipindi hiki. Je, serikali imepanga lini kwenda kuwafariji watu wale.

b) Lakini pia serikali imejipanga vipi kuwasaidia watu wale kwa kipindi chote hiki watakuwa hawana mavuno ya mpunga, ingawa nimeshazungumza na Mhe. Mohammedraza kwamba, kama Wizara ya Kilimo itafanya labda kumuomba au kukaribiana maana yake nimeshaongea nae yeye amejiamulia kutoa *packets* za mchele kwenda kuwafariji, na serikali je, itaongeza mchango wake katika sehemu hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, wizara tayari imeshajenga uzio wa maji ya chumvi mitatu kwa kupitia Mradi wa *TASAF* na serikali. Kwa hiyo, pindi fedha itakapopatikana basi yataendelea kujengwa hayo mengine.

Mhe. Spika, nategemea Mhe. Mwakilishi wangu ameridhika na kama hajaridhika naomba arudie tena lile swali lake jengine.

Mhe. Suleiman Sarahani Said: Mhe. Spika, swali langu la nyongeza la (b) linasema kwamba nilishaongea na Mhe. Mohammedraza, kuwa atatoa mchango wa kwenda kuwafariji watu wale kwa kutoa *packets* za mchele kwenda kuwasaidia kwa vile hawana kilimo cha mpunga. Je, na serikali itashirikiana na Mhe. Mohammedraza na mimi mwenyewe kwenda kusaidia kwa kutoa mchango kwa wale walioathirika na mabonde hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, serikali itakuwa tayari kwenda kumsaidia kutoa kwa sababu hiyo itakuwa ni kama sadaka tu.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa ruhusa yako, naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, mimi naipongeza serikali kwa nia njema kabisa ya kuwajali wakulima wake, lakini nije hapo hapo kwa muda huu na wingi wa hali ya maisha ilivyopanda kulimwa bure najua suala hilo litakuwa gumu kwa serikali kuchukua moja kwa moja isipokuwa inaongeza ufanisi tu kwa njia nyengine. Tatizo lilokuwepo sasa hivi

ambapo wakulima wetu wanalalamika kwa muda mrefu ni ukosefu wa matrekta katika maeneo mbali mbali bonde la Cheju, Kilombero, Upenja, mabonde ya Pemba na Kibokwa ni maeneo muhimu ambayo tunategemea kama yatapata mapema hayo matrekta kufanyiwa kazi basi mazao ya mpunga yataongezeka. Je, wizara ina mpango gani kuona suala la matrekta ni kuinua uchumi wetu wa kilimo ili wakulima wetu wasaidiwe.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Fedha imeshasaini mkataba wa Kampuni ya Mahindra and Mahindra *Limited* kwa ajili ya kuongeza matrekta ili uondokane na usumbufu wa hayo matrekta kidogo, kwa sababu tunayo matrekta 45 lakini yanayofanyakazi sio matrekta 45.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Spika, ahsante naomba kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Naibu Waziri. Kwa kuwa serikali inagharamika sana kununua matrekta ambayo bei yake ni kubwa. Je, kwa wale wote waliokabidhiwa haya matrekta au sekta maalum iliyokabidhiwa wanachukuliwa hatua gani kwa uharibifu wa yale matrekta kwani matumizi yao ni mabaya na matrekta ni bei kubwa sio kila siku serikali inunue tu wanachukuliwa hatua gani kwa hawa wanaoharibu haya matrekta.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ni kwamba haya matrekta yapo wizarani na yapo katika Idara ya Kilimo na trekta moja linapofanya kazi basi lazima lirudi kufanyiwa *service* na *service* yake ni gharama kidogo. Kwa hiyo, si kama labda wanaharibu ama vipi, chochote kitumiwacho huisha.

Nam. 55

Kutokufanyika kwa Tamasha la Mzanzibari

Mhe. Nassor Salim Ali - Aliuliza:-

Katika miaka ya nyuma kulikuwa na tamasha kubwa la Mzanzibari lakini katika miaka ya hivi karibuni tamasha hilo halifanywi tena.

a) Je, ni sababu gani zilizo sababisha kutofanyika kwa tamasha hilo.

b) Je, serikali haioni kuwa kutofanyika kwa matamasha kama hayo ni kurudisha nyuma utamaduni wa Kizanzibari na vijana kukosa kujua mila na silka zetu za Kizanzibari.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishsi swali lake Nam. 55 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Mhe. Rais wa Zanzibar ilitangaza kuwa kila ifikapo tarehe 19 Julai mpaka tarehe 25 kila mwaka tuadhimishe kuwa ni juma la wiki ya Utamaduni wa Mzanzibari.

Mhe. Spika, kwa sababu miaka mitatu iliyopita 2012, 2013 na 2014 Tamasha hili halikufanyika, kutokana na kuingiliana na Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na hivyo kupelekea kusitisha kwa muda maadhimisho hayo hadi mwaka jana 2015 tulipolirudisha tena baada ya kukamilika kwa Mfungo wa Ramadhani.Tunatarajia kwa mwaka huu litakuwepo kama kawaida katika mwezi wa Julai.*(Makofi)*

(b) Mhe. Spika, serikali inakubaliana na maoni ya Mwakilishi kuwa kutofanyika kwa matamasha haya kunarudisha nyuma utamaduni wa Mzanzibari ambapo itapelekea vizazi vijavyo kutokujua mila na silka zetu.

Mhe. Spika, ninachotaka kulihakikishia Baraza lako tukufu ni kwamba, Serikali ya Zanzibar inayoongozwa na Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein inaendelea kuhakikisha kwamba matamasha haya yanafanyika kama kawaida.*(Makofi)*

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mbali na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri, lakini kwa kuwa Tamasha la Utamaduni la Mzanzibari pamoja na matamasha mengine ambayo ameyataja ambapo likiwepo Tamasha la Mangapwani, Tamasha la Vyakula Asilia vya Makunduchi kwa Maalim Haroun Ali Suleiman, Tamasha la Kojani pamoja na Tamasha la Pete. Matamasha haya huwa ni kivutio kikubwa cha watalii kuja Zanzibar katika kuangalia utamaduni wetu.

Je, wizara imechukua hatua gani kuyatangaza matamasha haya ambayo yote nimeyataja kuitangaza Zanzibar na kuweza kuyajua matamasha haya ili kuwa kivutio kwa watalii kuyatangaza ndani ya nchi na nje ya nchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi, nakubaliana naye kwamba tamasha letu la Zanzibar ni tamasha ambalo linaitangaza Zanzibar kiutamaduni, kiutalii na mambo mengineyo. Hatua tuliyochukua au iliyochukuliwa na serikali kupitia wizara yetu ili kuyatangaza matamasha haya duniani na kwengineko, tumejiandaa au tumejipanga kuyatangaza matamasha haya kupitia sehemu tofauti ulimwenguni. Kwa mfano, pia tumeandaa Matamasha ya Jahazi ambayo yanawashirikisha wadau kutoka nchi mbali mbali. Kwa hiyo, huu ni ushahidi tosha kwamba serikali inachukua juhudi kuyatangaza matamasha yetu ya Zanzibar na watalii kuja kujionea matamasha haya.*(Makofi)*

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika, ahsante na mimi ningependa kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Niseme tu kwamba haya matamasha yamekuwa yakizungumziwa sana na watu tofauti ndani ya jamii pamoja na viongozi wetu mbali mbali. Kuna matamasha makubwa ambayo hapa inakuwa yanafanyika kwa muda wa miaka zaidi ya 10, moja yao likiwa Tamasha la Majahazi, maarufu *Zanzibar International Film Festival* na pia Tamasha la Sauti za Busara. Na mimi nikiri tu kwamba hapa pasiwe na *conflict of interest*, kwa sababu mimi pia ni Mwenyekiti Muanzilishi, kwa hiyo, nazungumza kabisa kwa nia njema. Lakini matamasha haya kila siku zikienda kama kwenye swali la msingi lilivyosemwa hapa kwamba yamekuwa yanapata changamoto hasa katika masuala ya kifedha...

Mhe. Spika: Mheshimiwa, uliza swali.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika ahsante.

(a) Mhe. Spika, ni lini wizara yake itakuja na mpango maalum kuanzisha Mfuko maalum wa kusaidia matamasha kama haya au kusaidia mambo ya sanaa.

(b) Kuna matamasha tayari yako hatarini kutoweka kutokana na uhaba wa fedha kama Sauti za Busara na mengineyo kama yalivyotajwa katika swali la msingi. Je, serikali haioni umuhimu wa kuingilia kati ili kuhakikisha hayo maneno yanayozungumzwa kwenye masuala ya utalii pamoja na utamaduni kuunganisha (*cultural tourism*) hapa kuingilia kati na kusaidia kifedha. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

(a) Mhe. Spika, namhakikishia na kumthibitishia Mhe. Mwakilishi kwamba, tumejipanga kama nilivyojibu katika swali mama,

tumejipanga kuanzisha matamasha mbali mbali na kuitangaza Zanzibar kwa watalii au kwa dunia nzima ili kuja katika nchi yetu na kuyaona matamasha haya.

(b) Nakubaliana na yeye kwamba matamasha yana umuhimu mkubwa na nimhakikishie kwamba umuhimu huu bado tutaendelea kushirikiana na serikali ili haya Matamasha ya Busara na mengineyo yaendelee. Kwa sababu pia inaitangaza nchi yetu kiutalii na kiutamaduni, hivyo, nimthibitishie Mhe. Mwakilishi umuhimu huu na mimi nauhitaji pamoja na wizara na serikali na inaona haya matamasha ni muhimu kwa kuitangaza Zanzibar. Kwa hiyo, tutaendelea kuyapa umuhimu matamasha haya kwa kuyaendeleza.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, swali la mwisho la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri, amekiri kwamba hivi sasa utamaduni wa Kizanzibari umerudi nyuma na kwamba vijana wamekosa kujua mila na silka zao, na kwa kuwa tunajua kuwa moja ya sababu ambayo inasababisha kurudi nyuma kwa utamaduni wa Kizanzibari ni matumizi ya mitandao kwa vijana ambao huiga maisha ya Kimagharibi (*Western Culture*).

Je, serikali haioni kwamba ipo haja sasa ya kudhibiti mitandao hasa ile ya *social media* kama jirani zetu wa Uganda wamekuwa wakifanya.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kwanza naungana na Mhe. Mwakilishi kwamba, kama nilivyojibu katika swali mama kuwa utamaduni wetu kama hatutouendeleza mila na silka zetu za Kizanzibari zitapotea na vijana wetu kupoteza kujua silka zao za Kizanzibari. Lakini nataka nikiri kwamba mitandao inatuharibia watoto wetu wa Kizanzibari au kijamii na kidunia kwa jumla. Hii pia inapelekea vijana wetu kuiga mambo ambayo hayafai.

Kwa mfano, vijana wetu sasa hivi tumewaona badala ya kuvaa suruali panapotakiwa wanavaa chini ya matako, wakati huu sio utamaduni wetu na silka zetu za Kizanzibari. Kwa hiyo, nimhakikishie Mhe. Mwakilishi, tutachukua jukumu hili au tutakuwa na mapango maalum tukishirikiana na serikali kuidhibiti hii mitandao kwa kuwaondoshea watoto wetu kuiga mambo yasiyostahiki kwa Wazanzibari. Ahsante. *(Makofi)*

Nam. 66

Uthibiti wa Matendo ya Udhalilishaji

Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Aliuliza:-

Tarehe 6 Disemba, 2014 Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliongoza kampeni kubwa ya kupinga vitendo vya Udhalilishaji na Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto ambapo Mhe. Rais alitoka na kauli kubwa ya "Udhalilishaji sasa basi", kauli ambayo iliungwa mkono na kila mtu ndani na nje ya Zanzibar. Kwa kuwa miaka miwili imepita sasa, tangu Mhe. Rais kuzitaka taasisi husika na serikali kuchukua hatua zinazofaa za kupambana dhidi ya vitendo hivi.

Ni kwa kiasi gani (kitakwimu) vitendo vya Udhalilishaji na Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto vimepungua Zanzibar kwa kipindi hicho tangu Mhe. Rais alipoingilia kati suala hili.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa heshima napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 66 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza napenda kumtanabahisha Mhe. Mjumbe kuwa kampeni hiyo ilizinduliwa tarehe 6 Disemba, 2014 ambapo hivi sasa ni mwaka mmoja na nusu tangu kuanzishwa kwake.

Mhe. Spika, tokea uzinduzi wa Kampeni, wizara imepata mashirikiano makubwa kutoka kwa baadhi ya wadau na taasisi mbali mbali Unguja na Pemba kuhakikisha kuwa janga hili linatokomezwa kama Mhe. Mjumbe, alivyosema.

Mhe. Spika, napenda kuvipongeza Vyombo vya Habari kwani vinachukua jitihada kubwa kuielimisha jamii katika Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Jumla ya vipindi 180 vimeandaliwa na kurushwa katika redio ya *ZBC*, Redio Jamii, *Zenj FM* na Televisheni. Pia, jumla ya sehemu 100 za Mchezo wa Mshike Mshike zimerushwa hewani zinazolenga kuelimisha jamii namna ya kupambana na kuchukua hatua za kuzuia vitendo hivi visiendelee katika jamii yetu.

Vile vile, jumla ya viongozi wa dini 39 wamepatiwa mafunzo ya ukufunzi kwa kutumia miongozo ya dini ya kupambana na vitendo hivi iliyotayarishwa na wizara ambapo hivi sasa wanahamasisha jamii juu ya namna ya kuzuia na kuchukua hatua za kupambana na vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia katika mikusanyiko ya kidini na vyombo vya Habari. Viongozi wa dini ya kikristo wameunda mtandao maalum wa kuelimisha jamii inayowazunguka Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, wanaume nao hawako nyuma katika kampeni hii ambapo mtandao wa wanaume umeundwa na unafanya kazi ya kuielimisha jamii kupitia maskuli, misikiti, madrasa na katika Shehia za Unguja na Pemba. Mtandao huu umepitia karibu Skuli zote za Msingi Unguja na Pemba kuelimisha juu ya namna ya kuzuia na kujikinga na janga hili.

Kamati za Shehia za kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia zinachukua jitihada kubwa ya kuelimisha na kufuatilia mienendo ya kesi katika shehia zao. Jumla ya Kamati 20 Unguja na Pemba zimepatiwa mafunzo juu ya namna ya kupambana na vitendo hivi na mafunzo haya yanaendelea hatua kwa hatua kwa kamati zilizobakia. Kamati hizi zimeandaa Mipango Kazi ya namna ya kulisimamia suala hili katika shehia hizi.

Mhe. Spika, kutokana na jitihada zinazofanyika, mwamko wa jamii umekuwa kwa kiasi katika kuripoti matukio yanayohusiana na ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto. Jumla ya malalamiko 100 (46 Unguja na 54 Pemba) ya wanawake walioripotiwa wizarani kwa mwaka 2015 na jumla ya matukio 170; (Unguja 114 na Pemba 56) yanayohusu udhalilishaji wa watoto yameripotiwa katika Idara ya Wazee na Ustawi wa Jamii.

Pia, jumla ya matukio 840 (Pemba 82 na Unguja 758) yameripotiwa katika vituo vya Mkono kwa Mkono. Kwa matukio ya Unguja (kukashifiwa 284, kubakwa 369 kulawitiwa 15 na Ujauzito 90) yaliyoripotiwa katika Kituo cha Mkono kwa Mkono Mnazi Mmoja. Pia, jumla ya simu 475 zimepokelewa zinazotaka huduma mbali mbali kuhusiana na kadhia hii, kati ya hizo simu 18 zinahusu udhalilishaji wa wanawake na watoto na zimepatiwa rufaa sehemu mbali mbali na simu zilizobaki zinauliza maswali mbali mbali yasiyohusiana na hayo.

Mhe. Spika, takwimu kutoka Mahakamani zinaonyesha kuwa mnamo mwaka 2014, jumla ya kesi 96 zilifunguliwa zinazohusu ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto, kati ya hizo kesi 5 zilitoewa uamuzi na kesi 24 zimetupiliwa mbali na kesi zilizobaki zilikua zinaendelea. Pia, kuanzia Januari

hadi Oktoba 2015, jumla ya kesi 49 zilifunguliwa na kati ya hizo ni kesi 2 tu zilizopatiwa hukumu na 47 zilikua zinaendelea. Katika Mahakama ya Watoto, jumla ya kesi 64 zilifunguliwa kwa mwaka 2015; kati ya hizo kesi 55 zilitolewa uamuzi na kesi 9 zinaendelea.

Mhe. Spika, hali hii inasikitisha sana na inavunja moyo kuona kuwa ni kesi chache tu zinazopatiwa hukumu.Wizara bado haijafanya utafiti tokea kampeni hii izinduliwe, ili kuweza kuelewa kwamba vitendo hivi vimepungua au vimezidi. Lakini kwa mtizamo wa haraka haraka wa kuongezeka kwa matukio yanayoripotiwa inaonekana vitendo hivi vinazidi badala ya kupunguwa. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii nimulize Mhe. Waziri, swali la nyongeza. Kabla sijauliza naomba nimpongeze waziri kwa majibu yake mazuri, lakini pia niunge mkono jitihada ambazo serikali imezifanya juu ya kuona kwamba hili tatizo linaondoka na hivi sasa inaonekana kwamba tatizo limehama mitaani lakini limehamia Mahakamani.

Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri kwa kuwa katika kampeni ile kuliahidiwa kupatiwa mashine ya *DNA* ambayo ingerahisisha usikilizwaji wa kesi hizi za ubakaji. Nilikuwa nataka kujua suala lile limefikia wapi.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, suala la *DNA* linafanyiwa utaratibu wa kupatikana, lakini ni kwamba taratibu za *DNA* zinakawia sana kwa sababu mtoto lazima azaliwe kwanza akishazaliwa ndio itapatikana damu ya mtoto na baba ili aweze kufanya hivyo. Kwa hiyo, utaratibu pia unabidi kusubiri na yule aliyekuwa ameathiriwa anaendelea kusubiri katika mazingira magumu.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, na mimi nina swali moja lenye (a) na (b). Kwa jitihada za serikali za kupunguza unyanyasaji wa kijinsia, nimeona serikali jitihada zake ziko nje zaidi. Sasa mimi namuuliza Mhe. Waziri.

(a) Katika ndoa kuna mikataba ya Kiisilamu ambayo inafungwa wakati wa ndoa, lakini wakati wa kuvunjia ndoa mikataba ile mingi sana huwa inaishia kinyemela. Je, serikali imejipangaje baba anapoamua kumuacha mama au kumfukuza kwa kipindi chote alichokaa nacho na kumvumilia na kila aina ya hali mbaya. Je, serikali imejipangaje kumpatia haki yake mama huyu.

(b) Serikali imejipangaje kwa sababu yule baba anapomuacha anamuacha na watoto wanaenda mitaani kuharibika. Je, serikali imejipangaje

kuchukuwa matumizi ya yale watoto au huduma za wale watoto kutoka kwa baba kwa kipindi chote mpaka wafikie miaka kumi na nane.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, nafurahi sana anayeuliza kwamba ni mwanamme na kwa taratibu na naamini kabisa sijui kama ana wazo la kupata mke wa pili. Lakini kama ana mke mmoja nitaendelea kumshauri kwamba abaki na mke mmoja ili aweze kutulelea watoto wazuri katika taifa la Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nataka kusema kwamba suala hili ni suala ambalo linahusu masuala ya imani na dini na itikadi zake kwa pande zote mbili. Kwa upande wa wakristo wanasema mke ni mmoja na hawaruhusiwi kuachana. Kwa hiyo, suala hili linakuwa si tatizo sana.

Lakini wa upande wa kiisilamu ninavyofamu kwa elimu ndogo ni kwamba baba anaoa na anaruhusiwa kuacha anapewa nafasi za wanawake wanne. Lakini suala ulilolitoa wewe ni zuri sana na limenifariji sana kwa sababu bado ni suala ambalo linatakiwa kutolewa mawazo katika vyombo husika vinavyotoa sheria hasa vile vya kidini ili viweze kuona ni jinsi gani tutaona tatizo hili na kuweza kuchangia. Lakini bado nyinyi ndio watunga sheria kwa upande wa Tanzania Bara nadhani mwanamke akishakaa na mume kwa muda wa miaka miwili wakiachana lazima wagawane mali zote zile sawa sawa. (*Makofi*)

Lakini kwa Zanzibar bado sheria ya ndoa iko kwenye masuala ya kidini, lakini bado nyie kama watunga sheria labda mgeweza kutafuta utaratibu muafaka utakaoweza kutusaidia kwamba huyu baba anapokwenda kuanza kuoa mke wa pili basi akumbe kwamba mtu aliemlisha vidagaa, aliemlaza kwenye magodoro ya viti, aliemnunulia kanga kwenye mitumba, aliemsaidia yeye kuchangamka kujenga nyumba na kununua gari ni mke wa kwanza. (*Makofi*)

Kwa hiyo, basi kuwe na utaratibu kabisa wa kusema kama huyu bwana anajihisi ana nguvu za kutosha kupata mke wa pili, hasa anapokuwa anapata neema basi mali zote za kwanza muachie mke wa kwanza. Halafu yeye kama anampenda huyo mwengine na huyu kama anampenda kweli wakaanze kuchachatika kutafuta utaratibu mwengine wa kutafuta maisha yao wenyewe. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nataka kusema hili liko mikononi mwenu na ni changamoto, naomba niwarudishie mtusaidie ili ni jinsi gani tuweze kulitengeneza. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Ahsante Mhe. Spika, kwanza na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Pili, nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ametujibu na mimi kama mwanamke nimesema nisimame na nimuulize Mhe. Waziri, kuhusiana na hizi kesi za unyanyasaji.

Tumeona kesi hizi za nyanyasaji au udhalilishaji ni suala TAMBUKA linatugusa kwa namna mmoja au nyengine, kama haijakugusa wewe basi imemgusa jirani yako, kama haijamgusa jirani yako basi imemgusa ndugu yako. Katika kesi hizi Mhe. Waziri, ametupa majibu kwamba kuna kesi nyingi ambazo zimewasilishwa lakini kesi chake sana ambazo zimetolewa majibu.

Je, Mhe. Waziri wizara yako inatwambiwa nini au imejipangaje kwenye kesi za kuzimaliza na kuliondoa tatizo hili la unyanyasaji hapa Zanzibar. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, pia, napenda kushukuru pia kuwa alieuliza ni mwana mama mlezi ambaye namba moja katika jamii. Kwa sababu ninachoamini kabisa mama ndio mlezi wa kwanza katika familia, yeye huyu anakuwa ni askari, huyu mama pia anakuwa mwanasheria, huyu mama anakuwa mtibabu na huyu mama pia ni mshauri namba moja kwa watoto.

Labda niseme tu kwa kuanzia na mama kwamba mama anahusika sana katika suala la kumlea mtoto. Jambo ambalo limeliona mpaka sasa hivi imeonesha wazi kwa kuwa watoto hawapewi ulinzi unaotosha na hawafatiliwi ipasavyo wanapokuwa wadogo na lile suala la kuvunjika ndoa watoto wanapolelewa na mama wa kambo au majirani ile mila ya kufatilia mtoto wa jirani anapoonekana katika mazingira magumi yameachiwa, yaani wamepuuzwa.

Lakini nataka kukwambia tu kwamba hilo jambo mimi linaniuma sana kupita kiasi na mara nyengine nakosa usingizi kwa sababu najua kabisa mtoto anapoathirika akidhalilishwa ni sawa sawa na madawa ya kulevya. Kwa sababu nafsi yake inakuwa imeumizwa hana jambo kasema ana-*lose confidence* katika jamii anaonekana kama ni kituko, kumbe yeye ndie aliefanyiwa kituko, mfanyaji anaonekana kama ni mtu sijui niseme neno gani zuri zaidi, anaonekana kama ni bora zaidi au amekuwa ni mtu hodari katika kufanya mambo yale.

Kwa hiyo, wizara kutokana na hali halisi inajitokeza mahakamani na kwenye vyombo vinavyohusika kushirikiana na wizara zote zinazohusika ina mkakati wa makusudi wa kupanga kuangalia jinsi gani tutaweza kuhakikisha kwamba tunatoa vile vipengele vyote vinavyoruhusu kukimbizwa kwa kesi, kwa sababu kesi ya unyanyasaji na udhalilishaji kwa hali niliyoiona haiko katika kifungu kimoja mbacho kimekidhi masuala yote, imechukuliwa tu, imenyofolewa nyofolewa kwa kutoka kipengele hiki kuweka kwenye kipengele hiki.

Nyengine ni ya mwaka 1917 ya masuala ya ushahidi, ushahidi mwengine unamwambia kwamba huwezi kumuhukumu mtu mpaka uone kile kitendo kinafanyika. Ndugu zangu ni lini watu wanapotaka kufanya kitendo wakafanya kitendo hadhara kama ngombe na kuku? Mara nyingi hujenga mazingira ya kujicha.

Kwa hiyo, suala la kumkuta mtu *ready-handed*, yaani ana kwa ana kama sheria moja ya kiislamu inavyosema kwamba umkute mtu anafanya kile kitendo na amwite mtu mwengine na mwengime ili waweze kushuhudia. Hasa utaona hizo ni sheria ambazo nadhani lazima tuzifanyie kazi ya makusudi ya kuhakikisha kwamba zinakaa katika mazingira yaliokuwepo.

Mimi kwa binafsi ningependa kusema kwamba pia sheria ya kuona kwamba ushahidi ni pamoja mazingira uwezo kuchukuliwa kama ni tatizo mojawapo la kuweza kumaliza hizi kesi mapema. (*Makofi*)

Nam. 19

Kuwekwa matuta barabara ya Dunga mitini

Mhe. Simai Mohamed Said - Aliuliza:-

Kwa kuwa eneo la Dunga Mitini kumekuwa na mtindo wa magari madogo ya mizigo na makubwa ya mchanga kwenda mwendo wa kasi na kuhatarisha maisha ya watu.

Je, ni lini Serikali itajenga matuta ya kupunguza mwendo kasi ili kukinga ajali na kunusuru maisha ya watu wa eneo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 19 kama ifutavyo:-

Mhe. Spika, kwa sasa serikali haina mpango wa kujenga matuta katika eneo hilo na badala yake itaweka michoro ya barabarani pamoja na alama zitakazowaongoza madereva wa magari hayo kupunguza mwendo kwa sababu tayari imeshaweka matuta katika eneo la Skuli ya Dunga na Skuli ya Uzini ambapo pana wanafunzi wengi na kuendelea kuiwekea barabara matuta kila sehemu litaondoa lengo la kujenga barabara la kurahisisha usafirishaji wa abiria na mizigo.

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpaka basi): Ahsante Mhe. Spika, ni wajibu wa serikali kuwalinda wananchi wake wakati wowote. Eneo la Dunga ni eneo linaloitwa ni *T-junction*, magari yanayopita ni magari ya mawe, mchanga, magari ya kawaida na yanakwenda kwa mwendo wa kasi mkubwa sana. Lakini pale kuanzia eneo la *nursery* Dunga Bweni hadi Dunga Kiembeni *nursery* pana watoto, vijana, wazee, watu wazima wanavuka barabara, ni eneo la hatari kwa kweli na si dhani majibu aliyoyatoa Mhe. Naibu Waziri kwamba kuweka alama za barabarani zitaweza kusaidia. Mimi ningependa kumuuliza Mhe. Naibu Spika.

(a) Je, endapo katika hili eneo la Dunga utakuwa uko tayari kwenda kufanya utaratibu mzima kuangalia na kuwahoji wananchi ili ulipe kipaumbele la kuzingatia kama kweli panawezekana pakajengwa matuta kuliko kulikataa moja kwa moja kuweka alama za barabarani.

(b) Lakini pia eneo la Dunga Kiembeni *nursery* pana matatizo kama hayo kwa sababu ni watoto wengi wanaopita. Lakini katika maeneo hayo yote pamoja na Tunguu na Kaebona kuna matatizo kama haya ambayo magari yanakwenda kwa mwende wa kasi. Hasa ni vizuri tukaangalia kwa pamoja uwezekano katika jinsi gani serikali itaweza kusaidia na kuwalinda wananchi wake. Mimi ningependa kumsisitiza kwamba...

Mhe: Spika: Mheshimiwa, uliza swali.

Mhe. Simai Mohamed Said (**Mpaka basi**): Je, Mhe. Naibu Waziri, utakuwa uko tayari kwenda kutusaidia na kuangalia uwezekano wa kujenga matuta?

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, tujuavyo sote kwamba Sheria za usalama barabarani ni muhimu kwa madereva wote kuzitii pale ambapo pana alama zinazowekwa. Lakini hata hivyo, kwa vile sisi tunapenda kujali maisha ya watu wetu hasa watoto wadogo kama sehemu za mashule, hata vituo vya afya huwa tunaweka matuta. Sasa niko

tayari kwenda kuangalia sehemu hiyo na iwapo itaonekana kuna haja ya kuweka matuta basi wizara yangu haitosika kufanya kazi hiyo. (*Makofi*)

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Spika, Zanzibar ni nchi moja ambayo madereva wanasababisha ajali za kizembe kila siku na kuuwa wananchi na hii ni kutokuwa na vituo vya gari za abiria barabarani.

(a) Je, wizara yako ina mpango gani ya kuweka vituo vya gari za abiria barabarani ili kupunguza ajali za kizembe Zanzibar.

(b) Barabara Mhe. Spika, zinajengwa kila siku nzuri, imara na madhubuti lakini hazima maegesho au vituo maalum vilivyoingia vya mkato vya kusimama gari za abiria. Je, wizara yake hizi barabara zote wana mpango gani kuziwekea maegesho maalum la kusimama gari za abiria.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, Kama unavyofahamu kwamba sio kwamba vituo vya daladala kuwepo au maegesho ya gari kuwepo yanasababisha ajali. Nataka kumpa mfano mzuri tu kwamba Mikoa ya Kusini na Kaskazini Pemba ndio Mikoa ambayo ajali zake ziko chache sana na wala huwezi kukuta kwamba kuna vituo vya daladala maalum vimewekwa.

Wakati hapa Mjini Magharibi ndio sehemu ambayo kuna vituo vya daladala zimewekwa lakini inaongoza kwa ajali na zimepatikana ajali 450. Kwa hiyo, mimi nachukuwa nafasi hii kwanza kuwapongeza madereva wa Pemba kwani wanaonesha wako makini sana katika kazi zao na katika mikoa hiyo utakuta kwamba Kaskazini Pemba kulikuwa na ajali 21 lakini vifo 11 na Kusini Pemba kulikuwa na ajali 23 vifo 5.

Wakati Mkoa wa Kusini Unguja ndio uliongoza kwa vifo kukaonekana kuna vifo 44 na Mjini Magharibi vifo 39. Kwa hiyo, moja kwa moja ni umakini tu madereva na kutii na sheria za usalama barabarani.

Kuhusu kuweka vituo hivyo vya daladala tunasema tunachukuwa shauri lake na tutalifanyia kazi *inshaallah*. (*Makofi*)

Mhe. Hussen Ibrahim Makungu (Bhaa): Mhe. Spika, kwanza nampongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana na kwa ufanisi mkubwa kwa kujibu kweke. Lakini pia nimshukuru Mhe. Waziri sana Baraza la juzi

alikiri kwamba kuna barabara yangu moja kutoka Mwanyanya, Sharifu Mssa, Bububu kuwa serikali itatia lami barabara ile mimi nashukuru sana.

Mhe. Spika, nasema hivyo, kwa sababu imeshatiwa kifusi mara mbili, fedha nyingi serikali imepoteza mara ya kwanza na mara ya pili na sasa hivi njia ile imeshaharibika tena. Kwa hivyo, namshukuru Mhe. Waziri na serikali sana kwa nia yake njema.

(a) Barabara hii itatiwa lami lini, naomba anambie jibu la uhakika ili nipate kujua barabara hii ili iondoshe usumbufu kwa wananchi wangu.

(b) Pale Mshelisheni Kibweni kuna karo au msingi wa kupita maji ambao walijenga Kajima kipindi cha miaka mingi inafika miaka 20 nyuma. Mvua ya juzi kusema kweli Mhe. Spika, maji yalikwama kutokana na ile tundu ya kupita maji kwenda pwani ilikuwa ni ndogo, kazi hiyo hiyo ilifanywa pale kwenye barabara ya Kibweni Hospitali ya KMKM ilipasuliwa barabara na ikaengezwa makalbi ili ile njia iwe kubwa. Sasa pale Mshelishelini pale nia bado...

Mhe. Spika: Swali Mheshimiwa.

Mhe. Hussen Ibrahim Makungu (Bhaa): Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, hiyo barabara inaweza kufanyiwa kazi lini na kama inaweza kufanyiwa kazi mimi binafsi chini wa wizara yake milioni tano nitasaidia ili barabara ile ikatwe ili kuondosha usumbufu wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

(a) Mhe. Spika, kwanza barabara yake tumeiona kwamba ina kipaumbele kikubwa sana hasa kunapotokea matatizo kama yalivyotokezea hivi karibuni ya barabara kukatika pale kutokana na mvua kubwa kunyesha. Kwa hiyo, iko katika kipaumbele chetu na ninamuahidi kwamba katika kipindi cha miaka mitano ya ilani yetu tutahakikisha kwamba ile barabara tunaitengeneza kwa kutumia lami na *inshaallah* atusubirie tu kwani kuna barabara nyingi tumezipa kipaumbele na zikiwa tayari moja baada ya moja tutazifanyia kazi.

(b) Napokea sana ushauri wake na vile vile na mapendekezo yake ya kututolea milioni tano kuanza hiyo kazi na sisi kwa kupitia wahandisi wetu tuko tayari kufanikisha hiyo kazi. Ahsante sana. (*Makof*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, maswali yamemalizika na kwa bahati mbaya hatuna matangazo ya wageni, kwa hiyo, leo hatuna wageni wowote.Waheshimiwa, nilipewa taarifa kwamba kidogo wakati mnapokuwa mnaingia kunakuwa na msongamano lakini unatokana na baadhi ya walinzi wenzetu hawa wanaotokea nje ya Baraza kwamba hawawafahamu Waheshimiwa.

Mimi ninachokifanya labda ni kukukumbusheni tu kwamba mna vitambulisho vyenu basi muvitumie ili kuepusha kusongamana pale ili muweze kupewa kipaumbele kuweza kuingia ndani kabla ya wangi.

Taarifa nyengine niliyonayo ni ya masikitiko kidogo kuna mwenzetu Mhe. Zulfa Mmaka, amepatwa na mkasa jana wameingia wezi kwake wakamuibia. Kwa hiyo, alitaka nikupeni taarifa ili muweze kujua namna ya kumfariji.

Katibu kwa shughuli zinazoendelea tafadhali. Samahani subiri kuna utaratibu.

Utaratibu

Mhe. Spika: Haya Mhe. Wanu Hafidh Ameir, kanuni.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, naomba kutumia kanuni ya 63 sambamba na kanuni ya 59(8) kutaka muongozo wako. Wakati Mhe. Naibu Waziri wa Habari, akinijibu swali langu alisema kwamba ni kweli utamaduni wa Kizanzibari umeshuka lakini akatumia neno kwamba vijana siku hizi wanavaa suruali chini ya "Matako" lugha ambayo haifai katika Baraza. Naomba Mhe. Naibu Waziri, ama afute kauli yake ama azingatie kwamba lugha kama hizi hazitumiki katika Baraza, naomba muongozo wako Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Wanu Hafidh Ameir. Waheshimiwa labda tukumbushane tu Wajumbe sote pamoja na Waheshimiwa Mawaziri wazingatie lugha za staha kidogo wanapokuwa wanachangia au wanapokuwa wanajibu. Hata mimi nililisikia lile neno lakini ninadhani kuna neno la Kiswahili ambalo linaweza likapoza uzito wa neno lile. Kwa hivyo neno lile lisitumike badala

yake litumike lile neno ambalo ni afadhali kwa jamii. Watu wanatuangalia. Mwalimu Haroun yupo mara nyingi sana huwa anatukumbusha matumizi mazuri ya Kiswahili. (*Makofi*)

Kwa hivyo, neno kama lile lisitumike. Ahsante sana Mhe. Wanu Hafidh Ameir, kwa muongozo wako, lakini ni funzo kwetu sote kwamba tujaribu kutumia lugha za staha. Na Kanuni ndivyo inavyotaka.

Ahsanteni sana Waheshimiwa.

Katibu tuendelee.

MUONGOZO

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Spika, ahsante na mimi ningependa kutumia Kanuni Nam. 37 (1) inayosema kwamba, "Waziri au Mjumbe yeyote anayeulizwa swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu, usahihi na kwa ufupi".

Mhe. Spika, wakati ninauliza swali langu la Nam. 52 kwenye orodha ya kazi za leo Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo majibu aliyotoa sikuridhika nayo, sikutaka tu pale kumuingilia pale pale kati kati. Lakini nikahisi ni vyema shughuli za kazi ziendelee. Kwa hivyo ningeomba muongozo wako Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Samahani hujafahamu, hukuridhika naye kwamba kajibu swali silo ulilouliza au vipi. Jaribu kufafanua kidogo ili tukuelewe.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 37 (1) inasema kwamba "Waziri au Mjumbe yeyote anayeulizwa swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu, usahihi na kwa ufupi".

Majibu ya swali la nyongeza nililouliza, majibu niliyopata hayaendani kabisa na swali nililoliuliza.

Mhe. Spika, ahsante sana na ninaomba muongozo wako.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, mimi naomba nimshauri Mhe. Simai Mohamed Said. Kama hakuridhika na jibu lililotolewa na Mhe. Naibu Waziri basi aliulize

tena, alilete kwa utaratibu au amuandikie kwa maandishi huyo Waziri ili amjibu kwa maandishi ili aridhike, halafu baadae jawabu lolote liletwe hapa. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante labda umesaidia hicho hicho ambacho nimetaka kumfahamisha Mhe. Simai kwamba kuna utaratibu kama unakuwa hukuridhika umtake Waziri akuletee kwa maandishi, au Waziri mwenyewe pia akihisi kwamba sina majibu ambayo yanatosheleza swali ambalo ameulizwa, yeye ataji-*commit* kwamba nitakujibu kwa maandishi.

Na yameshatokea hapa Mawaziri wanatoa *commitment* ya kujibu kwa maandishi. Kwa hivyo ninafikiri ni utaratibu mzuri zaidi kwamba mtu hakuridhika na lile swali, hivyo linajibiwa kwa maandishi. Na lile linalojibiwa kwa maandishi kikawaida liwafike Wajumbe wote kwa utaratibu huo huo, na siyo wewe uliokuwa hakuridhika tu, lakini Wajumbe wengine wote wapate majibu yale ambayo yatakuwa ni ya maandishi.

Ahsante naomba sasa tuendelee Waheshimiwa. Katibu tafadhali.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato) ya 2016

(Kusomwa kwa Mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, kama ilivyo ada Serikali kila mwaka ifanye mapitio ya mfumo wa kodi kwa nia ya kuimarisha mfumo huo. Matokeo ya mapitio hayo ni marekebisho ya sheria mbali mbali za kodi kupitia Sheria ya Fedha.

Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Fedha kwa 2016 unawasilishwa ili kufanyia marekebisho Sheria sita zilizotajwa katika Mswada huo.

Mapendekezo na marekebisho yamezingatia haja ya kuongeza mapato ya Serikali, kuendeleza ulipaji kodi wa hiyari, maoni ya wadau, maeneo ya ukuzaji na malipo ya kodi kwa bidhaa na huduma zinazoingizwa Zanzibar.

Madhumuni na Sababu

Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Kutoza Fedha ya 2016 unalenga kubadilisha baadhi ya vifungu vinavyohusiana na ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya

Serikali ili kuzifanya Sheria hizo kuwa bora zaidi na kuziba mianya mbali mbali. Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa ni hizi zifuatazo:-

1. Sheria Nam. 7 ya 2009 ya Usimamizi wa Kodi *(Tax Administration Procedure Act).*
2. Sheria Nam. 4 ya 1998 ya Ongezeko la Thamani (*VAT*).
3. Sheria Nam. 11 ya 2014 ya Uimarishaji na Uendelezaji Vitega Uchumi.
4. Sheria Nam. 8 ya 2006 ya Mafunzo ya Amali.
5. Sheria Nam. 9 ya 2015 ya Fedha.
6. Sheria Nam. 1 ya 2006 Rufaa za Kodi.

Mhe. Spika, sababu za marekebisho yanayopendekezwa ni pamoja na hizi zifuatazo:-

1. Kuziba mianya iliyobainika ya kupoteza mapato katika sheria husika.
2. Kupunguza mzigo wa uwajibikaji kwa walipa kodi kwa kuwaongezea muda wa uwasilishaji hati za kodi (*return*).
3. Kuweka bayana utaratibu wa malipo ya kodi kwa huduma zinazoingizwa Zanzibar na kutozwa kodi ya ongezeko la thamani (*VAT*).
4. Kuainisha taasisi zaidi zinazopendekezwa kusamehewa kulipa kodi ya *Steel Development Revenue.*
5. Kutekelezwa kwa matakwa ya Sheria ya Fedha za Umma Nam. 12 ya 2005 kuhusiana na usimamizi wa mapato ya Serikali.
6. Kuweka utaratibu mzuri zaidi wa uteuzi wa Mrajis wa Mahakama za Rufaa za Kodi.

Mhe. Spika, Mswada huu unatimiza masharti ya Kifungu cha 133 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 kinachozuia kutozwa kodi ya aina yoyote isipokuwa kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi na masharti mengine.

Maeneo ya Marekebisho

Mhe. Spika, Mswada umeainisha mapendekezo ya marekebisho ya Sheria za Kodi za Fedha kwa mwaka 2016. Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni hizi zifuatazo:-

1.Sheria ya Usimamizi wa Kodi Nam. 7 ya 2009 kwa kurekebisha mambo yafuatayo:-

(i). Kurekebisha Kifungu cha 18 kwa kubadilisha tarehe ya uwasilishaji wa hati za kodi (*return*) kuwa tarehe kumi ya kila mwezi badala ya tarehe saba iliopo sasa. Lengo la hatua hii ni kutoa muda wa kutosha kwa wafanyabiashara kufunga hesabu zao kwa mauzo ya mwezi uliopita. Marekebisho yanatokana na mapendekezo ya wadau katika kikao cha Kamati ya Mageuzi wa mfumo wa kodi.

(ii). Ninapendekeza kurekebisha Kifungu (3) cha Kifungu cha 23 kwa kufuta maneno, "walipa kodi wote" na badala yake kuweka maneno, "aina fulani za biashara" ili kuweka muongozo mzuri kwa madaraka aliyopewa Kamishna chini ya Kifungu hicho.

(iii). Kufanyia marekebisho Kifungu cha 54(a) kwa kuongeza vifungu vidogo vya (3) hadi (9) ili kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali kwa biashara zinazoendeshwa na watu wengine wasiokuwa wamiliki.

Kwa sasa kumejitokeza mtindo kwa wawekezaji kuwaachia watu wengine kuendesha biashara zao kwa makubaliano maalum. Imejitokeza kuwa waendeshaji huacha madeni makubwa ya kodi na wazabuni mbali mbali bila ya dhamana yoyote ya kugomboa kodi hizo.

Chini ya marekebisho yanayopendekezwa itakuwa ni wajibu wa wanaokodishana kutoa taarifa kwa Kamishna (kwa maana anayekodishwa) na anayeendesha kuweka dhamana Bodi ya Mapato na dhima ya kodi inaweza kuhamia kwa anayekodisha pindi anayekodishwa akishindwa kulipa kodi kwa ukamilifu.

(iv). Kurekebisha Kifungu cha 52 (2) ili kutoa mamlaka kwa Kamishna kuhukumu makosa mbali mbali hata bila ya kuombwa na mlipa kodi husika. Hata hivyo, Kifungu kipya pia kinatoa haki kwa mlipa kodi asiyeridhika kuwasilisha rufaa yake katika Bodi ya Rufaa za Kodi.

2. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Nam. 4 ya 1998. Kifungu cha 16 kwa kuweka uwazi zaidi sababu za mazingira yanayomfanya

mlipa kodi kujipunguzia kodi ya ununuzi na masharti yake. Marekebisho pia yanaweka utaratibu maalum wa utozwaji wa *VAT* kwa huduma zinazoingizwa. Sheria ya sasa kwa bahati mbaya haina utaratibu huo.

3.Sheria ya Fedha Nam. 9 ya 2015. Sheria hii inafanyiwa marekebisho, kufanya marekibisho Kifungu cha 20 (3) ili kuwezesha kodi ya miundombinu kwa wageni wanaolala katika hoteli kulipa ama kwa Dola moja au kiwango kinachofanana kwa shilingi ya Tanzania. Kwa sasa Sheria imetamka tu Dola moja na hivyo kuleta usumbufu kwa hoteli ndogo ndogo zinazolipisha wageni kwa shilingi.

4.Sheria ya Mafunzo ya Amali Nam. 8 ya 2006, kwa kurekebisha Kifungu cha 15 kwa kutoa msamaha wa kulipa kodi ya kukuza ujuzi *(Skills Development Revenue)* kwa taasisi za Kibalozi na Umoja wa Mataifa na mashirika yake. Kwa sasa ni taasisi za Serikali tu ndizo zinazopokea fedha kupitia Mfuko Mkuu ndizo zinazosamehewa rasmi kodi hiyo. Marekebisho pia yanataka taasisi zinazolipa ada hiyo kuwasilisha hati za kodi (*return*) kwa Naibu Kamishna wa *TRA* mara mbili kwa mwaka na kutoa taarifa za malipo haya.

5.Sheria ya Vitega Uchumi (*ZIPA*) Nam. 11 ya 2004 kwa kurekebisha Kifungu cha 20(1) kwa kuweka udhibiti zaidi wa misamaha ya kodi kwa kuongeza ngazi ya Waziri katika utiaji saini kwa shahada za uwekezaji zenye misamaha ya kodi.

Pili, marekebisho yanapendekeza kuwepo kwa mashauriano baina ya Waziri na Waziri wa sekta husika pale panapokuwa na mashauriano ya kutolewa vivutio zaidi ya vile vilivyotajwa katika jadweli ya sheria. Aidha, anapotokea kuwa Waziri anayesimamia Vitega Uchumi ni tofauti na Waziri wa Fedha marekebisho yanapendekeza kuwa kwa vivutio vinavyohusu mapato ya Serikali lazima mashauriano yafanywe baina ya Waziri mwenye dhamana ya fedha na Waziri anayehusika na sekta hiyo. Lengo la hatua hii ni kulinda mapato ya Serikali na kuhakikisha ushirikishwaji wa sekta zinazohusika.

6.Sheria ya Rufaa za Kodi Nam. 1 ya 2006. Hapa inapendekezwa kubadilishwa Kifungu (1) cha Kifungu cha 14, kwa kuweka madaraka ya uteuzi wa Mrajis kwa Mhe. Jaji Mkuu badala ya Waziri

wa Fedha. Utaratibu unaopendekezwa unaendana na utaratibu uliopo wa uteuzi wa Mrajis kwa taasisi zenye hadhi ya Kimahakama na unalenga kuweka uwajibikaji zaidi kwa Mrajis.

Mapendekezo:

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba Baraza lako Tukufu liupokee, liujadili na hatimaye liupitishe Mswada wa Sheria ya Fedha ya 2016.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.(*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Mipango hoja imetolewa na naona imeungwa mkono.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja imetolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe sasa naomba hii hoja ijadiliwe. Kwa hivyo nitaanza sasa kumwita Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti ili naye aweze kuchangia. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa maoni ya Kamati ya Wenyeviti katika Mswada huu unaohusu Sheria ya Kutoza Kodi na kubadilisha baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi kuhusiana na ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya Serikali na mambo mengine yanayohusiano na hayo.

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kutujaalia kwa mara nyengine tena kukutana tukiwa na afya njema, pamoja na shauku ya kuendelea kutekeleza majukumu ya Kitaifa ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar, katika kuhakikisha tunapeleka mbele gurudumu la maendeleo.

Mhe. Spika, napenda pia kuchukua fursa hii, kuwapongeza Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi chini ya usimamizi wako Mhe. Spika, kwa umakini mkubwa kabisa kumaliza kuichangia na kuichambua hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Serikali, Mwelekeo wa Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017, uchangiaji ambao unaonesha kwa kiasi gani Wajumbe wa

Baraza hili wana shauku ya kuhakikisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, inakuwa na mipango mizuri na yenye kutekelezeka katika kukuza uchumi wa Zanzibar, kupunguza umasikini na kuhakisha huduma muhimu za kijamii zinapatikana kwa wananchi katika ubora unaoridhisha na gharama zinazoendana na hali za kimaisha za wananchi wetu.

Mhe. Spika, shukurani zangu pia ziende kama nilivyosema kwa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Khalid Salum Mohamed, pamoja na jopo lake zima la wataalamu kwa matayarisho mazuri na kutuwasilishia kwenye Kamati yetu Mswada huu wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi kuhusiana na ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya Serikali na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, pamoja na kutumia muda wao, kukaa na Kamati ya Wenyeviti, kujadili mswada huu kwa pamoja na kutupatia ufafanuzi muafaka katika maeneo mbali mbali ya mswada huu ambayo kwa namna moja au nyengine yaliwatanza Wajumbe na kuhitaji ufafanuzi ili kuuelewa Mswada huu vizuri zaidi.

Mhe. Spika**,** kabla ya kwenda moja kwa moja kwenye mswada huu, ningependa kuwapongeza Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Wenyeviti ambao tulifanya kazi bega kwa bega katika kuhakikisha zoezi la kuupitia mswada huu linakamilika kwa wakati na kwa ufanisi mkubwa. Kwa ruhusa yako Mhe. Spika, naomba niwatambue kwa majina yao kama ifuatavyo;-

1.	Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame	-	M/Mwenyekiti
3.	Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Mjumbe
4.	Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Mjumbe
5.	Mhe. Machano Othman Said	-	Mjumbe
6.	Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Mjumbe
7.	Mhe. Omar Seif Abeid	-	Mjumbe

Wote kwa kweli tunawapongeza na tunawashukuru sana kwa mashirikiano mazuri tuliyoyafanya katika kuupitisha Mswada huu. Sitowasahau Makatibu wetu wawili, nao ni:

1. Ndg. Nasra Awadh Salmin	-	Katibu; na
2.Ndg. Kassim Tafana Kassim	-	Katibu

Uchambuzi wa Mswada

Mhe. Spika, lengo la mswada huu wa Sheria kama alivyoeleza Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa ujumla ni kuondoa mapungufu mbali mbali ya kiutendaji na kiutekelezaji ambayo kwa upande mwengine yangeweza kuwapa mwanya walipa kodi wasio waadilifu kutokutekeleza wajibu wao kisheria wa kulipa kodi, lakini pia mswada huu unadhamiria kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali ili kwenda sambamba na azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuhakikisha inasimamia ipasavyo mapato ya ndani.

Mhe. Spika, tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuandaa Mswada wa Sheria utakaotoa fursa ya malipo mbadala kupitia thamani ya kubadilisha dola iliyopo, kwa kulipia dola moja ya kimarekani au malipo yanayolingana na hayo kwa shilingi ya kitanzania kwa mtu mmoja kwa siku katika malipo ya kodi ya miundombinu. Kamati yangu imefurahishwa sana na marekebisho haya kwa ujumla, kwani inadhihirisha jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuhakikisha inapunguza mahitaji ya matumizi ya dola kwa matumizi ya ndani na hatimaye kupunguza kasi ya kupungua thamani kwa Shilingi ya Tanzania.

Kamati yangu inaipongeza Serikali na mamlaka husika kwa kufikiria marekebisho haya ambayo kwa muda mrefu imekuwa ni kilio cha wahusika yaani "*Stakeholders*".

Mhe. Spika, Kamati ya Wenyeviti inaunga mkono pia mapendekezo ya Mswada ya kutoa fursa na muda zaidi kwa mlipa kodi ambapo mlipa kodi sasa atafanya malipo ifikapo tarehe kumi ya kila mwezi badala ya tarehe saba kama ilivyokuwa awali.

Mhe. Spika, tunaunga mkono hili kwa kuwa wafanyabiashara wengi walikuwa wanasikitika kuwa muda uliowekwa ni mdogo.

Mhe. Spika, sambamba na hayo, kamati yangu inaipongeza serikali kwa kuweka bayana tafsiri ya neno "mmiliki' kwani hapo kabla endapo Afisa wa Mapato atakwenda kukusanya kodi katika sehemu fulani basi yule mtu anayemkuta husema yeye sio mmiliki. Kitendo hiki kilikuwa kinawapa usumbufu maafisa wanaokusanya kodi, endapo mswada huu utapita na kuwa Sheria, mtu yeyote atakayekutwa katika eneo la biashara basi atabeba jukumu la kulipa kodi.

Mhe. Spika, kamati yangu kwa umakini mkubwa iliupitia mswada huu muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu na kuibua marekebisho mbali mbali kama yanavyoonekana kwenye Waraka wa Kamati. Baadhi ya marekebisho hayo ni pamoja na marekebisho ya kisarufi ambapo vifungu mbali mbali vilirekebishwa kwa lengo la kuviwezesha kusomeka vyema na kuleta dhamira iliyokusudiwa.

Mhe. Spika, baadhi ya vifungu hivyo ni kifungu cha 8 ambacho kimerekebishwa kwa kuongezwa maneno **'**moja ya nyaraka zifuatazo;' mwishoni mwa kifungu kidogo kipya cha (4) pamoja na kufutwa neno 'au' liliopo mwishoni mwa aya (a) na (b).

Vile vile, marekebisho ya kisarufi yalipendekezwa kwenye kifungu cha 13(a) cha mswada katika kifungu kidogo kipya cha (2)(b) kwa kufutwa neno 'kawaida' na badala yake kuwekwa neno 'kudumu' kwenye kifungu.

Mhe. Spika, marekebisho mengine ni kama yanavyoonekana kwenye waraka wa mapendekezo ya marekebisho ya kamati hii kuhusiana na Mswada huu yaliyogaiwa kwa Wajumbe wa Baraza.

Mhe. Spika, Kamati ya Wenyeviti pia ilipendekeza kufutwa kwa baadhi ya vifungu vya Mswada huo kwa kuwa vifungu hivyo vilionekana havina msingi wowote. Baadhi ya vifungu vyenyewe ni kifungu cha 5 cha mswada ambacho kinapendekeza kuongezwa kifungu kidogo kipya cha (8)(c) cha kifungu cha 54A cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi Namba 7 ya 2009, pamoja na kufutwa kifungu kidogo kipya cha (11) cha kifungu cha 54A cha Sheria hiyo.

Mhe. Spika, marekebisho mengine yaliyopendekezwa na kamati hii ni kuweka usawa wa maneno baina ya Mswada wa Kiswahili na Mswada wa Kiingereza ili miswada hii iendane. Mfano wa vifungu vilivyobainika kuwa na marekebisho hayo ni kifungu cha 12 cha mswada kinachorekebisha kifungu cha 15(4) cha Sheria ya Mafunzo ya Amali Namba 8 ya 2006, ambapo katika Mswada wa Kiswahili vimekosekana vifungu vidogo vya (2) na (3), katika kifungu kidogo hicho cha (4) wakati katika Mswada wa Kiingereza vimetajwa vifungu vidogo hivyo.

Sambamba na kifungu cha 15(b) cha mswada kinachorekebisha kifungu cha 20 cha Sheria ya Ukuzaji Vitega Uchumi Namba 11 ya 2004 kinachoongeza kifungu kidogo cha (1)(b), ambacho kimependekezwa sasa kisomeke; 'Waziri anayehusika na fedha ataweka saini hati iliyotajwa kwenye aya (a) ya kifungu hiki'.

Mhe. Spika, vile vile, kamati yangu imependekeza kuandikwa upya baadhi ya vifungu kwa kuwa mpangilio wake unaleta utata kwa msomaji. Vifungu vyenyewe ni kifungu cha 6 cha Mswada kinachorekebisha kifungu cha 56 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi pamoja na kifungu cha 13 cha mswada kinachorekebisha kifungu cha 29 cha Sheria ya Mafunzo ya Amali.

Mhe. Spika, mpangilio wa vifungu hivyo ni kama vilivyowekwa kwenye waraka wa mapendekezo ya marekebisho ya kamati.

Mhe. Spika, Kamati ya Wenyeviti pia ilifanya marekebisho ya Mswada wa Fedha kwa upande wa makosa ya kiuchapaji kwa lengo la kuweka bayana maneno yaliyotumika. Baadhi ya vifungu ambayo vilikuwa na makosa ya kiuchapaji ni kifungu cha 5 cha Mswada kinachoongeza kifungu kidogo cha (5)(a) cha kifungu cha 54A cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, kwa kufuta neno **'**kuazia' na badala yake kuweka neno 'kuanzia'. Pia, kwenye kifungu kidogo cha (5)(b) cha Sheria hiyo kwa kufuta neno 'yanayodaiwa' na badala yake kuweka neno **'**inayodaiwa'.

Hitimisho

Mhe. Spika, kwa ujumla niwapongeze Wajumbe wote wa kamati yangu ya wenyeviti kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuupitia mswada huu, licha ya upya wao, kwa kuweza kuuchambua, kupendekeza, kuhoji na kuibua hoja za kujenga kwa lengo la kupata sheria iliyo thabiti na inayohakikisha haimpi mwanya wa ukwepaji wa ulipaji kodi muhusika "*stakeholder*" yeyote au kumkandamiza kwa namna yoyote ile.

Mhe. Spika, ni imani yangu kwamba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili, watauchangia, wataujadili, na hatimaye kuupitisha mswada huu muhimu wa ukusanyaji mapato na kuendeleza nchi yetu, kwa lengo la kuleta ufanisi wa ulipaji kodi na ukusanyaji wa mapato ya serikali**.**

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti kwa kuwasilisha.

Waheshimiwa Wajumbe, kwa kuwa sijapata maombi kutoka kwa mjumbe yeyote kuendelea kuchangia hii hoja. Sasa naomba nichukue nafasi hii sasa

nimwite Mhe. Waziri ili kama ana chochote cha kuongezea kuhusiana na mchango wa Kamati ya Wenyeviti, ili aweze kutupa machache. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, tafadhali.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi na wajumbe wote, kwa michango yao na taarifa yao nzuri waliyoitoa na niseme naipokea taarifa iliyotolewa na kamati hiyo.

Vile vile niwashukuru wajumbe wote kwa kuielewa taarifa tuliyoiwasilisha. Mhe. Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Waziri wa Fedha wa Mipango. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango alipowasilisha alitoa hoja, imechangiwa na Mhe. Makamu Mwenyekiti, lakini sasa kabla hatujaendelea na sehemu nyengine, naomba sasa niwahoji kwa wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, halafu hatua nyengine zitafuata.

Sasa naomba kuwahoji wale wote wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Makamu Mwenyekiti wanyanyue mikono yao, wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, taarifa tafadhali.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kuupitia mswada huu kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mhe. Spika: Samahani kabla hatujaingia kwenye kamati, Mhe. Machano Othman Said.

UTARATIBU

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, utaratibu kidogo. Mswada huu ni muhimu sana katika kupitisha bajeti yetu, kwa bahati nzuri Waheshimiwa Wajumbe wengi wanakunywa chai sasa hivi. Kwa hivyo, ningeomba tu pengine utumie kiti chako kuwaarifu wajumbe waingie ndani ili tuje kupitisha mswada huu.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Machano Othman Said kwa kutukumbusha, nitawaomba wahudumu wa Baraza wapige kengele pamoja na kwenda kuwaita wajumbe kule waliko ili waweze kuja, tufanye kazi muhimu sana ya kupitisha hii sheria. Katibu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato) ya 2016

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu 1 Jina Fupi na Kuanza Kutumika

Sehemu ya Pili

Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi Namba 7 ya Mwaka 2009

Kifungu 2 Kusomwa
Kifungu 3 Marekebisho ya Kifungu cha 18
Kifungu 4 Marekebisho ya Kifungu 23
Kifungu 5 Marekebisho ya Kifungu cha 54A, pamoja na marekebisho yake
Kifungu 6 Marekebisho ya Kifungu cha 56, pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Tatu

Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Namba 4 ya mwaka 1998

Kifungu 7 Kusomwa
Kifungu 8 Marekebisho ya Kifungu cha 16, pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Nne

Marekebisho ya Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato) Namba 9 ya mwaka 2015

Kifungu 9 Kusomwa
Kifungu 10 Marekebisho ya Kifungu cha 20

Sehemu ya Tano

Marekebisho ya Sheria ya Mafunzo ya Amali
Namba 8 ya mwaka 2006

Kifungu 11 Kusomwa, pamoja na marekebisho yake
Kifungu 12 Marekebisho ya Kifungu cha 15
Kifungu 13 Marekebisho ya Kifungu cha 29, pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Sita

Marekebisho ya Sheria ya Ukuzaji Vitega Uchumi
Namba 11 ya mwaka 2004

Kifungu 14 Kusomwa
Kifungu 15 Marekebisho ya Kifungu cha 20, pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Saba

Marekebisho ya Sheria ya Rufaa za Kodi ya Zanzibar
Namba 1 ya mwaka 2006

Kifungu 16 Marekebisho ya Kifungu cha 20, pamoja na marekebisho yake
Kifungu 17 Marekebisho ya Kifungu 14

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali bila ya marekebisho. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante, Mhe. Waziri ametoa hoja, sasa naomba niwahoji.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Spika: Ahsante sana. Mhe. Waziri ametoa hoja. Sasa naomba niwahoji Waheshimiwa Wajumbe, wale wote wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato) ya 2016

(Kusomwa kwa mara ya tatu)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Fedha Usimamizi wa Mapato ya mwaka 2016, usomwe kwa mara ya tatu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Waziri ametoa tena hoja, na amesoma kwa mara ya tatu. Sasa naomba niwahoji kwa mara nyengine tena.

Waheshimiwa Wajumbe, wale wote wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hapa ndio mwisho wa sehemu yetu sisi ya kupitisha huu mswada wa sheria. Sasa zitafuata hatua zinazofuata za kwenda kusainiwa na Rais kuwa sheria, na baada ya hapo tutaanza kutekeleza hii sheria kama ambavyo tumeipitisha.

Napenda nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, na niwatakie kheri pamoja na watendaji wake katika kutekeleza vifungu vya sheria ambavyo tumevipitisha vya mswada huu wa sheria hivi sasa. Nashukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha. Katibu.

UCHAGUZI WA WABUNGE WATAKAOINGIA BUNGENI

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, shughuli iliyopo hapa mbele yetu sasa hivi ni ya uchaguzi wa wenzetu watano ambao watakwenda kutuwakilisha katika Bunge la Jamhuri ya Muungano.

Kwanza kabisa napenda kuwataka wasaidizi wetu humu ndani ya ukumbi, ili waweze kuwapigia kengele Waheshimiwa Wajumbe wote ambao wanapata chai, ili waje kushiriki katika shughuli hii ambayo ni muhimu sana.

Pili, napenda niwaambie kwamba katika uchaguzi huu kuna wagombea watano tu ambao wameletwa na Chama cha Mapinduzi. Wagombea hawa watano utaratibu utakaotumika ni wa kupigiwa kura ya ndiyo au hapana. Wako watano na napenda niwataje majina yao hapa. Kwanza kabisa ni;

1. Mhe. Machano Othman Said
2. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
3. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, na
5. Mhe. Amina Iddi Mabrouk. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, napenda pia nikukumbusheni kwamba kwa mujibu wa kanuni ya 76 Spika, katika uchaguzi huu hana kura, kwa hivyo mtapata idadi ya wajumbe ambao wapo. Kura ya Spika itafanyakazi tu pale inapotokezea mgombea amepata kura za ndio au hapana ambazo ziko sawa, labda nikisome hiki kifungu.

Kanuni ya 76 kwa kufuata masharti ya kifungu cha 83(2), mtu atakayekuwa anaongoza kikao cha baraza;

a) Ikiwa ni Spika, atakuwa na kura ya uamuzi tu na sio ya asili.
b) Ikiwa asiye Spika, atakuwa na kura ya uamuzi na ya asili kwa maana kwamba angekuwepo Naibu Spika, hapa angeweza kuwa na kura ya asili na atakuwa na kura ya maamuzi inapotokezea kufungana kwa kura.

Lakini kwa kuwa kiti sasa hivi kinaongozwa na Spika, sitakuwa mpiga kura katika uchaguzi huu, kwa maana hiyo sasa naomba wasaidizi wetu watupe hesabu ya idadi ya Wajumbe ambao wamo ukumbini ili tuweze kujua idadi ya wapiga kura halali ambao tutakuwa nao. Baada ya hapo tutaendelea, Katibu naomba unipe hesabu tafadhali.

Katibu: Mhe. Spika, wajumbe wote ni 84, lakini waliopo sasa hivi ni wajumbe 65.

Mhe. Spika: Wajumbe waliopo ni 65, lakini kila mjumbe ambae atakuwa anaingia ukumbini tutakuwa sasa tunapeyana taarifa kwamba kuna mjumbe amezidi, ili kuendelea kuzidi kuongezea kwenye hii hisabu. Baada ya hapo Katibu tupe utaratibu.

Katibu: Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe baada ya utaratibu wa kupata wagombea walioelezwa katika kanuni ya 145 ya Kanuni za kudumu za Baraza

la Wawakilishi, utaratibu unaofuata ni uchaguzi wa Wajumbe hao na tunayo orodha ya wagombea wa nafasi hizo ni Wajumbe watano kwa Chama cha Mapinduzi, ambao ndicho kitakachokamilisha matakwa ya kanuni ya 145 na 146.

Wajumbe wenyewe ni kama wafuatao:

1) Mhe. Machano Othman Said;
2) Mhe. Jaku Hashim Ayoub;
3) Mhe. Hussein Ibrahi Makungu;
4) Mhe. Wanu Hafidh Ameir na;
5) Mhe. Amina Iddi Mabrouk.

Mhe. Spika, wagombea hawa watapigiwa kura ya siri na kila mgombea kabla ya zoezi la kupiga kura atapewa nafasi ya kujieleza kwa muda usiozidi dakika tano. Wajumbe wanaweza kumuuliza mgombea masuala yasiyozidi matatu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo Wajumbe ambao ni wagombea wanaweza kwa ruhusa yako kupata nafasi ya kujieleza mbele ya Wajumbe wenzao kabla ya zoezi la kupiga kura, na katika zoezi la kupiga kura Waheshimiwa Wajumbe karatasi yetu ya kura ni moja ambayo itakuwa na orodha ya Wajumbe wote wanaopigiwa kura. Katika kila jina la mgombea kutakuwa kuna chumba ambacho mgombea unaweza kumchagua aidha kwa kuweka alama ya vema kwenye ndio au hapana. Utakuwa umeshamchagua au kumkataa mgombea unayemtaka. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe, kama ambavyo Katibu ameelekeza kura yetu itakuwa ni moja ambayo itakuwa na majina yote matano, lakini mara baada ya jina la kila mgombea kutakuwa na chumba ambacho aidha, utamtilia kura ya ndio au hapana. Ikitokezea mjumbe mmoja umempa kura mbili; umempa ya ndio na ya hapana, kura hiyo itakuwa imeharibika kwa Mjumbe yule ambaye utakuwa umempigia kura ya aina hiyo. Au kama chumba kikiachwa wazi bila ya kupigwa kura kabisa.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hapo kwa sababu nyote mumo kwenye *ballot* nilikuwa naomba sasa Wajumbe waanze kuja mmoja baada ya mmoja nitakuwa nawaita majina, lakini sasa sijui kama mnalazimika mtoke nje au mbaki sehemu zenu mlizopo, Waheshimiwa Wajumbe wabaki?

Wajumbe: Wabaki!

Mhe. Spika: Ahsanteni Waheshimiwa wajumbe kwa hivyo tunakubaliana Wajumbe wabaki sehemu walizopo, lakini nitawaita majina yao mjumbe

mmoja baada ya mwengine, ili aje mbele atajieleza kwa muda usiozidi dakika tano kila mmoja, baada ya hapo kama kutakuwa kuna masuali yasiyozidi matatu ataulizwa mjumbe huyo. Baada ya hapo sasa naomba Katibu.

Katibu: Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwamba mjumbe mmoja ameongezeka sasa ni wajumbe 66.

Mhe. Spika: Asante, nimepewa taarifa ya mjumbe mmoja ameongezeka, kwa hivyo wamekuwa wajumbe wote walio halali kwa kupiga kura ni wajumbe 66. Baada ya hapo sasa naomba nichukue nafasi hii kumuita Mgombea wa Mwanzo Mhe. Machano Othman Said ili aje ajieleze.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Baraza hili tukufu asalamu allaykum. Niliyesimama mbele yenu naitwa Machano Othman Said, Muwakilishi wa Jimbo la Mfenesini, nimegombea nafasi ya Ubunge kupitia nafasi tano za Baraza la Wawakilishi. Waheshimiwa Wajumbe kwa heshima kubwa naomba munichague ili pia nikawafanyie kazi ile ambayo kanuni yetu ya Baraza la Wawakilishi 146(5) kama inavyotaka.

Mhe. Spika, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe kwa heshima kubwa naomba kura zenu.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Machano Othman Said, maswali!

Mhe. Shehe Hamad Matar: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii, naomba nimuulize Mheshimiwa mgombea, yeye anatoka katika Baraza hili kuwakilisha katika Bunge je, ni utaratibu gani atakaotumia kuchukua mawazo yetu na sisi kuyapeleka Bungeni.

Mhe. Machano Othman Said: Kama nilivyoanza kueleza kuwa ukifuata kanuni 146(5) kinaeleza kwamba;

> "Wajumbe watano watakaochaguliwa na Baraza hili miongoni mwao watamchagua mmoja ili kuwakilisha kuja kutoa ripoti ya Bunge kwenye Baraza lakini pia kuchukua maoni ya Baraza kwenda kwenye Bunge"

Kwa hivyo mimi nitasimamia kwa kushauriana na wenzangu ili tuweze kuwakilisha vizuri kwa kupata maoni yenu. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa heshima kabisa, kwa jinsi ninavyokufahamu ni mtu mwenye uzoefu, umekuwa ukitoa mchango mkubwa sana katika nchi yetu, nataka kukuuliza tu na uniridhishe jinsi gani utaisaidia Wizara ya Wanawake, Watoto na Wazee katika suala zima la udhalilishaji, katika masuala mbali mbali. Kwa sababu suaala hili linasimamiwa na vyombo vya Muungano, naomba jibu.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, nashukuru sana, bahati nzuri katika Serikali iliyopita nilikuwa Waziri na nilibahatika pia nikateuliwa katika kamati ya kusaidia Serikali katika kuhakikisha kwamba watoto na wanawake hawadhalilishwi. Hayo aliyosema Mhe. Waziri tuliyabaini kwamba pamoja na nguvu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini kuna vyombo vya Muungano ambavyo vinashughulika moja kwa moja na kesi na kuvunja tatizo hili. Kwa hivyo nikipata fursa hii ya kuingia Bungeni nafikiri itakuwa kisu kimepata sehemu ya kwenda kuchinjia.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano,Ujenzi na Usafirishaji: Nashkuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na mimi kumuuliza suali Mhe. Machano Othman Said, kwa kuwa alikuwa na uzoefu sana katika Wizara ambayo mimi hivi sasa naifanyia kazi. Je, utaisadia vipi Serikali kuhakikisha kwamba mahusiano yaliyokuwepo baina ya sisi na wenzetu kule yanadumishwa kwa ajili ya maslahi ya Zanzibar.

Mhe. Machano Othman Said: Namshukuru Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa suala lake zuri. Mimi najiona kwamba ninao uzoefu, nashukuru Serikali yangu lakini pia nakishukuru Chama changu cha Mapinduzi nimekuwa mjumbe wa *NEC* tangu 2002, kwa hivyo mambo mengi ya Tanzania nayajua na kuingia kwangu Bungeni tutaendelea kushirikiana kujenga mashirikiano ya Serikali mbili. Pia kujenga mashirikiano ya mhimili wa Bunge na Baraza la Wawakilishi. Waheshimiwa naomba kura zenu za ndio.

Mhe. Spika: Sasa namuita Mhe. Jaku Hashim Ayoub, njoo ili upate kujieleza mbele ya Wajumbe. Kidogo Katibu.

Katibu: Naomba kutoa taarifa kwamba Wajumbe wameongezeka wawili, sasa hivi ni 68.

Mhe. Spika: Ahsante wajumbe wawili wameongezeka wako wajumbe 68 sasa. Mhe. Jaku mbele yako ni wapiga kura kwa nafasi unayogombea ya Ubunge

kutoka ndani ya Baraza la Wawakilishi, jieleze sio zaidi ya dakika tano, kama ukizipunguza sio mbaya baada ya hapo kunaweza kuwa na masuali matatu unawezakuulizwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, waheshimiwa wajumbe mwanzo kabla ya yote Assalamu Aleykum. Kwa jina naitwa Jaku Hashim Ayoub, Muwakilishi wa Jimbo la Peja, hapo mwanzo nilikuwa Muwakilishi wa Jimbo la Muyuni kabla ya kukatwa majimbo mapya. Kwa heshima kabisa nimegombea nafasi hii ya Ubunge kupitia Baraza la Wawakilishi kwa kipindi chengine cha pili na Mwenyezi Mungu akanijaalia na hizi jitihada nitakuwa si mwingi wa fadhila kama sikukushukuruni nyinyi Wajumbe mlionipa nafasi hii. Kabla ya kuendelea nikukushukuruni tena na tena kwa uungwana mlionionesha na kwa kuniamini kunirudisha tena kwa mara ya pili.

Kwa heshima kabisa Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako hili naomba kura za ndio katika nafasi hii, ili kwenda kumaliza ngwe iliyobaki kule kwa kipindi cha pili, ahsante sana.

Mhe. Spika: Maswali Mhe. Shamata nimekuona.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na mimi napenda nichukue fursa hii nimuulize Mhe. Jaku Hashim Ayoub, katika kipindi kilichopita nadhani ulikuwa mbunge kupitia Baraza hili hili la Wawakilishi katika nafasi tano, ningekuomba unieleze ni mambo gani ambayo uliyafanya katika kutekeleza majukumu yako kupitia Baraza hili la Wawakilihshi na vile vile ikaonekana kwamba umeweza kutekeleza majukumu yako kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nikushukuru sana Mhe. Shamata Shaame Khamis kwa suala lako zuri sana. Kazi niliyoifanya Barazani ni kubwa kama tunavyofahamu ikiwemo hasa sekta ya afya imepiga hatua ya maendeleo chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohammed Shein kwa jitihada alizozifanya, na muwakilishi pekee nafikiri kipindi kilichopita niliyeleta hoja binafsi kuisaidia Serikali katika sekta ya afya.

Kama haitoshi nije na suala jengine la Bungeni kwa faida ya Wajumbe vile vile na Bungeni nimefanya kazi kubwa sana hasa kunako sekta ya mambo ya Muungano, ahsante sana.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mgombea wetu Ubunge Mhe. Jaku Hashim Ayoub, naomba kumuuliza suala.

Mhe. Spika, tunaamini Waheshimiwa wanapochaguliwa hapa katika Baraza la Wawakilishi kwenda katika Bunge wanaliwakilisha Baraza pamoja na nchi kwa jumla, yaani nchi yetu ya Zanzibar. Na kwa kuwa kuna mambo mengi yanahitajika kupigiwa kelele au kuhamasishwa tupate misaada mbali mbali au mambo mbali mbali kwa manufaa ya Wazanzibari. Je, Mhe. Jaku unampango gani wa kuhakikisha kwamba kuna mambo ambayo yanaikabili Zanzibar kwa faida ya Wazanzibari kuyapigia kelele ili tufanikiwe.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kwanza niendelee tena na tena kumshukuru Mhe. Ali Suleiman maarufu (Shihata) kwa suala lako ambalo kama kuna wajumbe wanafuatilia bajeti iliyopita, ilikuwa suala la *FIFA* kugawa Dola laki mbili na nusu kwa Tanzania, Tanzania inaitwa Tanzania kutokana na Zanzibar.

Vile vile kuna pesa za *CECAFA* wanatoa Dola laki moja nikauliza suala hilo na bahati nzuri nikaambiwa niachie na nikaaeleza kuna Dola mbili na nusu Zanzibar, nilichokifahamu mimi kilichopatikana tokea kujiunga na *FIFA* ni uwanja wa Gombani kubandikwa nyasi za bandia. Suala hilo nimelifikisha kule si mara moja si mara mbili hata kwenye bajeti kuzuia mshahara, nikawambia maslahi ya Zanzibar katika mambo ya Muungano hatuna na nikawaambia uzoefu unaonesha Timu ya Tanzania inafungwa sana na Timu ya Zanzibar wakikutana.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza suala, Mhe. mgombea hebu nifahamishe kwamba katika Bunge ulikuwa mmoja wa wawakilishi kutoka Baraza la Wawakilishi na ulishindwa kuwakilisha ipasavyo Baraza hilo kwa mujibu wa kanuni ya 145(5). Je, unatushawishi vipi ili tujenge imani na wewe ili safari hii tukupeleke tana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kama kafatilia nazungumza kiswahili fasaha kabisa, kama kafuatilia hakuna muwakilisha aliyenikaribia mie katiba Bunge lile aliyeuliza masuala mengi kuliko mimi.(*Makofi*)
Mhe. Spika, kwa unyenyekevu wa hali ya juu kabisa, kwa heshima na taadhima naomba kura zenu za ndio, ili nikamalize kazi iliyobaki kule kikiwemo kiporo cha shamba letu la Makurunge.(*Makofi*)

Mhe. Spika: Sasa namuita Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, ili aje ajieleze mbele ya Wajumbe.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu mbele yako ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wewe ni mgombea nafasi ya ubunge kutoka katika Baraza la

Wawakilishi, nakuomba utumie muda wa dakika tatu mpaka tano kujieleza, baada ya hapo kutakuwa na masuali matatu ambayo utaulizwa na Wajumbe. Mwisho utaomba kura, ahsante sana.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru sana Aslamu alaykum. Kwanza awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu sote kwa kuwa hapa asubuhi hii salama na afya njema. Mimi mbele yenu naitwa Hussein Ibrahim Makungu ni Muwakilishi wa Jimbo la Mtoni kwa sasa, mwanzo nilikuwa muwakilishi wa Jimbo la Bububu, nashukuru wananchi wangu walinipa imani kubwa hasa wananchi wa Jimbo la Bububu. Na sasa wananchi wangu wa Jimbo la Mtoni pia wamenipa imani kubwa.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru sana kupata uzoefu mkubwa katika miaka mitatu hii niliyoongoza jimbo langu la Bububu na sasa hivi jimbo la Mtoni, lakini pia nilikuwa mjumbe wa Bunge maalum la Katiba, mwaka uliopita. Waheshimiwa wajumbe wote naomba kwa imani kubwa na wananchi wangu wa Jimbo la Mtoni walionionesha imani kwa kunichagua, lakini leo naomba kura hizi mbele yenu nyie Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa majimbo yote ya Zanzibar, naahidi mtaponichagua kuwa Mbunge wa Jamhuri ya Muungano kwa nafasi tano basi nitashirikiana kwa hali na mali na nyinyi kwa kusaidiana katika majimbo yenu kwa kazi ambazo zitakuwa na changamoto kwenu. Kwa hiyo, mimi ni sehemu ya wabunge lakini bilakupitia kwenu nyinyi siwezi kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, sasa naomba kura, nianze kwa Makamu wa Pili wa Rais, naomba kwa Mawaziri wote wa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar, pia kwa Manaibu Mawaziri na pia kwa Wajumbe wote wa Baraza hili la Wawakilishi naomba kura zao za ndio ili niweze kuwa Mbunge wa Jamhuri ya Muungano niweze kusaidiana nao, kushirikiana nao kwa kazi zote zinazohusiana na Zanzibar ili kwenda kusema Bungeni na waniongoze, sitokataa ushauri wao kwa hali na mali. Kama nilivyosema mwanzo imani kubwa wamenionesha lakini naendelea kuwaomba ili kuisaidia Zanzibar katika changamoto za Muungano zilizokuwepo. Mimi nitakuwa mjumbe wa kwenda kuisaidia kwa nia njema nchi yetu ya Tanzania katika masuala muhimu sana ya kimaendeleo. Waheshimiwa Wajumbe, naomba kura zenu za ndio ili niweze kuwatumikia wananchi kwa nia njema Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza swali Mhe. Hussein Ibrahim Makungu.

Mheshimiwa mgombea, kama inavyojulikana kwamba wewe ni miongoni mwa watu wanaofanya shughuli ngumu za biashara na vile vile ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi umeomba nafasi hii ngumu zaidi ya kwenda kutuwakilisha Bungeni, sijui utazifanya fanya vipi hizi kazi kwa wakati mmoja kwa sababu mara nyingi sana hivi vipindi vinaenda sambamba Bunge na Baraza la Wawakilishi ili kutuwakilisha ipasavyo ndani ya Bunge?

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa): Ahsante sana ndugu yangu kama ulivyosema mimi ni mmoja wa wafanyabiashara na nakuhakikishia kuwa nafahamu changamoto nyingi zilizokuwepo baina ya yetu sisi za ndani na za wenzetu Tanzania Bara. Kwa hivyo, naamini kabisa kukaa pamoja na wewe kutanisaidia pia kwa nia njema kwa kuisaidia nchi yetu kufikia yale malengo ambayo tuliyojiwekea.

Pia usione kama sifahamu ila nafahamu changamoto hizo mheshimiwa, na nitashirikiana na wajumbe wote kwa miongozo yao na busara zao ili niweze kuwawakilisha kule. Ahsante sana.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda nichukue fursa hii nimuulize Mhe. Hussein Ibrahim Makungu swali moja kama ifuatavyo. Mheshimiwa tunatarajia kwamba leo upo hapa unaomba kura, na nadhani wapiga kura watapima na wataona kwamba ni jinsi gani waweze kufanya maamuzi ili uweze kuwa Mbunge kama ambavyo unavyotarajia. Nilitaka nikuulize swali katika kipindi kilichopita tumeshuhudia matukio mbali mbali kwamba Muungano wetu ulitingisika kidogo au ulitikiswa miongoni mwa wajumbe waliokuweko kule Bungeni na miongoni mwa Wazanzibari waliweza kutingisika kwa wao kufuata mkumbo. Katika suala la Muungano mheshimiwa unatuhakikishia vipi na utashirikiana vipi na wenzako ili kuhakikisha kwamba katika hali hiyo tunaweza kupambana nayo isitokezee siku moja katika kipindi chako. Ahsante.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa): Mhe. Spika, kwanza nimwambie Mhe. Mjumbe mimi kwa suala la Muungano, mimi ni muumini wa Muungano asilimia mia kwa mia. Mhe. Mjumbe nasema kwa nia njema kwamba mimi ni muumini wa Muungano, niko hapa leo nina asili mbili; nina asili moja ya Kihindi na asili moja ya Kizaramu. Kwetu mimi ni Bagamoyo. Kwa hivyo, nasema hivi Waheshimiwa Wajumbe kwa dhati kabisa, ndio maana nilisema katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wakati wa kutunga Katiba Mpya inayopendekezwa kwenye Bunge Maalum mimi nilikuwepo na nilipiga kura zote za ndio kwa nia njema kabisa ya nchi yetu, na kama nitakuwa msaliti wa Muungano hata baba yangu huko aliko atakuwa hayupo radhi na mimi.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii naomba nimuulize Mhe. Mgombea; kwa kuwa Bunge la Jamhuri ya Muungano Tanzania lina mchanganyiko wa wabunge wa Bara na Visiwani na hasa kutoka kule Pemba, na ninavyoangalia katika mchango wao wa maendeleo Wabunge wanaotoka Pemba kutoka Chama cha Upinzani ni mdogo sana. Je, utalishawishi vipi Bunge kuhakikisha kwamba ile fedha inayotoka kutoka kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wakipewa Wabunge wa kule Pemba inatumika ipasavyo katika shughuli za maendeleo ya Zanzibar?

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa): Mhe. Spika, kama nilivyosema Mhe. Mjumbe mwanzo nitashirikiana na wewe kwa hali na mali na kuhakikisha Zanzibar inapata maslahi yake yote katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kila penye sehemu yake basi mimi nitakuwa mstari wa mbele ili haki yetu tuipate kwa kuwasaidia wananchi wetu na Zanzibar kwa ujumla. Kwa hivyo, Mhe. Mjumbe kwa suala lako hilo usiwe na wasi wasi, tutakaa mimi na wewe pamoja kama kuna mapungufu yoyote, mimi naamini wewe ndiye bosi wangu nitapokuwa mimi Mbunge basi mimi nitakuwa nakutumikia wewe zaidi na nitachukua ushauri wenu ili kupeleka Bungeni kwa nia njema na safi kabisa kwa ajili ya nchi yetu ya Tanzania. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Hussein Ibrahim Makungu omba kura halafu tuweze kumkaribisha mgombea mwengine.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa): Mhe. Spika, naomba kura kwanza kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais baba yangu, Waheshimiwa Mawaziri wote wazee wangu, wakubwa wangu walionitangulia, Waheshimiwa Wajumbe wote nakuombeni kura za ndio ili niweze kuwa Mbunge wenu niweze kukutumikieni kwa hali na mali katika Bunge miaka mitano hii ijayo. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Mhe. Wanu Hafidh Ameir mbele yako ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao ni wapiga kura katika nafasi uliyogombea ya Ubunge kutokea katika Baraza la Wawakilishi, una dakika tatu mpaka tano, jieleze na baada ya hapo utaulizwa maswali yasiyozidi matatu. Tafadhali omba kura Mhe. Wanu.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, ahsante, Wajumbe shikamoni.

Wajumbe: Marahaba.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Niliyesimama hapa naitwa Wanu Hafidh Ameir naomba ridhaa yenu kuliwakilisha Baraza hili katika Bunge la Jamhuri ya Muungano. Waheshimiwa Wajumbe naomba kura zenu.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa heshima napenda nichukue nafasi hii kumuuliza mgombea, binti mdogo ambaye anaonesha kabisa ana moyo wa kutaka kuchangia nchi yetu na kwa kipindi kifupi tu nimemsoma namba kwamba ni mchangiaji mzuri sana katika Baraza hili. Nataka anipe moyo na kunitia nguvu kwamba tutakapompa nafasi hii atakwenda kufanya kazi nzuri zaidi ya kuchangia kama anavyochangia hapa, hasa kwa ajili ya masuala ya wanawake, wazee, watoto, vijana na wengineo.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, ahsante naomba kumjibu Mhe. Waziri, kwanza nimshukuru kwa pongezi zake, lakini pili nimuhakikishie Mhe. Waziri pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote kwamba kasi ni ile ile kama nilivyo hapa basi nadhani Bungeni itakuwa zaidi ya hapa. (*Makofi*)

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Mhe. Spika, ahsante na mimi kwa kunipa fursa ya kumuuliza swali dada yangu Wanu, naamini kwamba Mhe. Wanu ni kijana mwenzetu, Mhe. Wanu tunamtegemea kwenye Baraza hili tukufu, tunaujua uwezo wake, tunamuamini na pia tunampenda. Kama vijana nilikuwa nataka nimuulize tunajua kwamba Bungeni kuna uwakilishi wa vijana tayari, lakini yeye kama kijana kwa sababu lazima tutie matumaini vijana wenzake atatuwakilisha vipi, atatushikia vipi bendera hii ili kuweza kutuwakilisha vyema kule. Ahsante.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, kwanza uwakilishi wangu kama kijana utaendelea kama ulivyo hivi sasa na hapa ndio mwanzo wa safari tu lakini huko mbele safari itakuwa kubwa zaidi.
Pili, nimjibu kwamba uwakilishaji wangu wa vijana katika Bunge utategemea sana mashirikiano yao vijana wenyewe watakayonipa katika kuwatetea masuala yao na matakwa yao katika Bunge.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Mhe. Spika, ahsante na mimi kwa kunipa fursa hii ya kumuuliza swali mgombea. Mhe. Mgombea unaomba kura ya Ubunge kwa kwenda kutuwakilisha sisi wawakilishi kule Bungeni, mimi ningependa utueleze mikakati yako ukijua wazi kwamba sisi wawakilishi kutoka Pemba tuna dhima kubwa kule Pemba ya kuwakilisha majimbo yetu. Sasa wewe kama Mbunge ambaye tunakupeleka kule utatusaidia namna gani kutuwakilisha

katika majimbo yetu sisi wawakilishi wa Pemba, ukitilia maanani kwamba kule ndio kuna upinzani mkubwa wa Wabunge wa CUF kule Bungeni. Ahsante sana.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, kwanza uwakilishi wangu katika Bunge utategemea masuala ambayo nitaenda kuwakilisha kwa maana ya kwamba kwa yale yanayohusiana na Muungano ndio ambayo nitasema kule katika Bunge. Lakini yale ambayo yanahusiana na majimbo yao hilo watanisaidia wao ili kuona mimi niwasaidiaje katika majimbo yao ya Pemba. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Wanu maswali kwa upande wako yatakuwa yamekwisha, omba kura halafu ukakae, nimkaribishe mwengine.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, naomba niombe kura kwanza kwa *frontbenchers*, lakini pili kwa *backbenchers* na pale kura zangu zitakapofungamana Mhe. Spika, naomba kura yangu uiangushie kwangu. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Wanu sasa naomba nimwite mgombea wa mwisho lakini si wa mwisho kwa umuhimu Mhe. Amina Iddi Mabrouk ili aje mbele yetu. Mhe. Amina Iddi Mabrouk, mbele yako ni Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao ni wapiga kura katika uchaguzi unaogombea wa kuliwakilisha Baraza la Wawakilishi kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano, una dakika tatu mpaka tano za kujieleza na kama watakuwa na masuala yasiyozidi matatu utaulizwa na baada ya hapo utaomba kura, ili waweze kukufikiria waheshimiwa.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Spika, ahsante sana.
Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako tukufu nikiwa mzima na afya njema.

Mhe. Spika, kwa jina naitwa Amina Iddi Mabrouk, Mwakilishi Viti Maalum Mkoa wa Magharibi. Mhe. Spika, nimesimama hapa kuomba kura za Waheshimiwa Wajumbe kwa kupitia nafasi ya Ubunge Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe naomba kura zenu za ndio ili ziniwezeshe kuwakilisha Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kama kuna maswali, mheshimiwa nakuona.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Amina Iddi Mabrouk swali langu kama ifuatavyo. Wabunge wengi wa Zanzibar wanapochaguliwa kwenda Bunge la Jamhuri ya Muungano huwa wengine wanamaliza miaka mitano bila ya kusimama kuzungumza kwenye Bunge la Jamhuri. Sasa nataka kukuuliza je, wewe utatuwakilisha vipi Baraza hili la Wawakilishi huko Bungeni?

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Mjumbe hilo ndilo lengo kuu la kunichagua katika Baraza hili la Wawakilishi ili niweze kuwawakilisha wawakilishi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, lakini jengine nitakapokuwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania siwezi kukurupuka tu kusimama bila ya kuwa na hoja ya msingi ya kuchangia. Mhe. Mjumbe nakuhakikishia kwamba pale nitapokuwa na hoja ya msingi basi nitasimama mbele ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili niweze kuwakilisha wawakilishi wa Baraza la Wawakilishi. (*Makofi*)

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi hii kumuuliza mgombea, yeye ameomba nafasi hii lakini pia ni mwanamke sasa ni vipaumbele gani ambavyo ameviweka kutusaidia ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano kama mwanamke mwenzetu, kwa sababu wanawake tuna changamoto nyingi.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Mjumbe, nafahamu kwamba sisi wanawake tuna changamoto nyingi na zinahitaji ufumbuzi, niahidi kwamba Mhe. Mjumbe nitakapokuwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na nyinyi wanawake basi nitahakikisha kwamba yale matatizo yanapungua kwa asilimia kubwa. (*Makofi*)

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na kuwa mtu wa mwisho kuuliza swali hili. Katika majibu ya jibu la awali alilokuwa anajibu Mhe. Amina na alisema ndani ya miaka mitano kwamba kuna suala hili la kukosa kile kitu cha kuchangia na tulichagua Wabunge hapa watano wakatuwakilishe na tuna uhakika miaka mitano waliitumia, kuna wengine hawakusimama hata siku moja. Hivi anatuthibitishia walikosa hoja ya msingi ya kuchangia kama ambavyo yeye alisema akikosa hoja ya msingi anaweza kuwa asichangie au akipata atachangia?

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Spika, samahani swali lake sijalisikia vizuri sijui kutokana na *mic* yake.

Mhe. Spika: Iwashe *mic* hiyo.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Naomba arejee.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Spika, naomba kurejea na nitarejea kwa ufafanuzi wa ziada kwamba tulichagua wabunge watano ndani ya chombo hiki kuliwakilisha Baraza kwenda katika Bunge la Jamhuri ya Muungano, lakini katika majibu yako ya awali ulisema kuwa utachangia pale utakapopata hoja za msingi. Je, unataka kututhibitishia kwamba wale wabunge watano tuliowapeleka maana kuna wengine hawakusimama hata mara moja walikosa hoja ya msingi ndani ya miaka mitano?

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Spika, swali lako Mhe. Mjumbe kwa kweli lina upana mrefu, mtu kukaa katika chombo hiki cha Baraza la Wawakilishi au Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutosimama kwa miaka mitano bila ya kuchangia haina maana kwamba wale waliochaguliwa hawana maana.

Mhe. Spika, nimuhakikishie Mhe. Mjumbe nitajitahidi sana nitapokuwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutumia Kanuni ya 146 ya Baraza la Wawakilishi kukusemeeni Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa nguvu zangu zote, ewe Mwenyezi Mungu nisaidie. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Amina omba kura.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Waheshimiwa Wajumbe, kwa heshima na taadhima, akina mama, Waheshimiwa Wawakilishi, akina baba, naomba kura zenu zote za ndio ili niweze kuwawakilisha katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ahsanteni.

Mhe. Spika: Katibu naomba utaratibu wa kuanza kugaiwa kura uanze, lakini kwanza tupewe hesabu ya idadi ya watu waliomo ndani maana yake niliona kama baadhi ya wajumbe wanatoka na kuingia.

Katibu: Mhe. Spika, mpaka hivi sasa tunao wajumbe 75 na tuko tayari kugawa kura.

Mhe. Spika: Haya utaratibu sasa wa kugawa kura, makatibu viko wapi visanduku vya kura. Kura zigawiwe, Katibu mbona kuna kisanduku kimoja tu cha kura zitatosheleza zote hizi?

(Hapa upigaji wa kura ulianza)

Waheshimiwa visanduku vitakufuateni hapo mlipo hamna haja ya kunyanyuka. Kwa wale ambao kura zao zitakuwa zimeharibika mtu anyooshe mkono halafu atafuatwa atapewa kura nyengine halafu hiyo iliyoharibika itachukuliwa na kuharibiwa mbele yake hapo.

Waheshimiwa Wajumbe mngesubiri kidogo kwanza baada ya kupiga kura msitoke, ningekushaurini msitoke kwanza.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwa wale wagombea ambao watataka kumteuwa mtu kwenda kuwakilisha katika zoezi la kuhesabu kura. Mhe. Machano Othman Said.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, ilivyokuwa majina haya yamewasilishwa Barazani na Chama cha Mapinduzi na mimi ni mgombea wa Chama cha Mapinduzi naomba nimteuwe Mnadhimu wa Chama cha Mapinduzi Mhe. Ali Salum Haji akasimamie kura zangu.

Mhe. Spika: Mhe. Machano Othman Said amesema kwamba Mnadhimu akasimamie. Sasa naomba niwaite na wagombea wengine kuwasikia, Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, na mimi nafuata nyayo hizo hizo za Mhe. Machano Othman Said kwa vile Mnadhimu wa Chama chetu cha Mapinduzi ndio asimamie shughuli hizo na mimi namuamini Mnadhimu wa Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Mhe. Spika, ahsante na mimi pia namchagua Mnadhimu wetu wa Chama cha Mapinduzi kwenda kunisimamia hizo kura zangu. Ahsante.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, namuamini Mnadhimu.

Mhe. Amina Idd Mabrouk: Mhe. Spika, na mimi niungane na wenzangu kwa kumuamini Mhe. Mnadhimu wetu cha Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Spika: Ahsanteni sana wagombea**.** Wagombe wote wanakubaliana kwamba watawakilishwa na mtu mmoja tu; Mnadhimu. Kwa hiyo, sasa nimuombe Mhe. Mnadhimu atoke mbele ili sasa aweze kufuatana na watendaji wetu katika zoezi hili la kwenda kuhesabu hizi kura. Karibu Mhe. Mnadhimu wa Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe baada ya zoezi hili naomba nisitishe hizi shughuli za Baraza mpaka baada ya kupata matokeo. Kwa hiyo, naomba tukatumie nje kiasi cha robo saa mpaka dakika 20 halafu tuweze kurudi tena hapa kwa ajili ya kupata matokeo. Yatakapokuwa tayari tutaitana ili tuweze kupeana matokeo. Baada ya hapo naomba kusitisha shughuli hizi.

(Saa 5:24 Baraza liliakhirishwa kwa muda wa dakika 15-20 kwa ajili ya kwenda kuhesabu kura)

(Saa 6:02 Baraza lilirudia)

MATOKEO YA UCHAGUZI

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tulisitisha kidogo shuhuli za Baraza ili kuwapata nafasi watendaji wetu kwenda kusimamia na kukamilisha mchakato huu wa matokeo ya uchaguzi ambao tumepiga hivi punde wa kuwapata Wabunge watano watakaoliwakilisha Baraza la Wawakilishi kule Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sasa napenda kuchukuwa nafasi hii kwanza kuwashukuru wale wote ambao wameshiriki katika huu uchaguzi Waheshimiwa Wajumbe. Niwashukuru kwa kutumia haki yenu kama wapiga kura ndani ya Baraza la Wawakilishi na baada ya hapo sasa naomba nitoe matoke ya uchaguzi wetu kama ifuatavyo:-

Wajumbe wote waliohudhuria wakati wa kupiga kura walikuwa Wajumbe 75 na Wajumbe waliopiga kura kati ya Wajumbe wote waliohudhuria ni Wajumbe 75 hivyo hivyo. Kwa hiyo, Wajumbe wote wamepiga kura.

Kura zilizomkubali Mhe. Amina Idd Mabrouk kati ya hizo ni kura 67, kura zilizoharibika mbili (2) na kura zilizomkataa ni sita (6). (*Makofi*)

Kura zilizombukubali Mhe. Mhe. Jaku Hashim Ayoub ni kura 58, kura zilizoharibika ni moja (1) na kura zilizomkataa 16. (*Makofi*)

Kura zilizombukubali Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) ni kura 63, kura zilizoharibika ni moja (1) na kura zilizomkataa ni 11. (*Makofi*)
Kura zilizomkubali Mhe. Machano Othman Said ni kura 72, kura zilizoharibika hakuna na kura zilizomkataa ni tatu (3). (*Makofi*)

Kura zilizombukubali Mhe. Wanu Hafidh Ameir ni kura 70, kura zilizoharibika ni mbili (2) na kura zilizomkataa ni kura tatu (3). (*Makofi*)

Kwa hivyo basi, Mhe. Amina Idd Mabrouk, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, Mhe. Machano Othman Said na Mhe. Wanu Hafidh Ameir wote wa CCM, wamechaguliwa kuwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi cha mwaka 2016 hadi 2020. Kwa hiyo, wote watano ni Wabunge halali kutokea ndani ya Baraza la Wawakilishi. (*Makofi*)

Mimi nichukue nafasi hii kuwapa pongezi za dhati kabisa na kuwataka watuwakilishe kama ilivyosema kanuni, wakatuwakilishe kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano kama ni Wabunge kutokea Baraza la Wawakilishi. Lakini pia napenda niwakumbushe kwa mujibu wa kanuni ya 145 fasili ya 5 ambayo inasema kama ifuatavyo:-

> "Wajumbe watano watakaochaguliwa na Baraza kwa mujibu wa kanuni hii watamchagua Mjumbe mmoja miongoni mwao kuwasilisha katika Baraza namna walivyoliwakilisha Baraza katika Bunge kwenye mkutano wa Baraza wa mwezi wa Machi au wakati mwengine ambao Baraza litaona inafaa".

Kwa mujibu wa kanuni hii maana yake ni kwamba, wao watano wakae na miongoni mwao wakubaliane ni nani atakayekuwa kiongozi wao kwa ajili ya kuifanya kazi hii muhimu kwa ajili ya Baraza la Wawakilishi.
Nichukuwe tena nafasi hii kuwapa pongezi sana na kuwaomba kwamba sasa waende kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wakatuwakilishe kama walivyoahidi wenyewe walipopewa nafasi ya kujieleza hapa mbele yetu. (*Makofi*)

Baada ya maneno hayo Waheshimiwa Wajumbe labda nichukue nafasi hii kila mmoja wao nimpe angalau dakika mbili ili aweze kutoa neno la shukurani baada ya kukamilika kwa huu uchaguzi. Naomba sasa nimwite Mhe. Machano Othman Said ili atoe neno la shukurani.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uchaguzi wa salama, uchaguzi ambao umeleta umoja na mshikamano katika Chama chetu cha Mapinduzi.
Lakini nikushukuru wewe Mhe. Spika kwa busara zako kwa kuongoza Baraza hili, niwashukuru Waheshimiwa wenzangu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa imani yao kwetu, kazi hii tumeimaliza lakini ndio tunainza kazi.

Mimi na wenzangu wanne kwa ujumla wetu watano tunawashukuru sana. Lakini kama Mhe. Spika, ulivyonukuu vifungu vya kanuni kifungu cha 145 fasili ya 5 na vifungu vyengine, tutajitahidi kufanya mageuzi katika uwakilishi wetu. Tutajitahidi kufanya kazi kwa pamoja tutasaidiana, tutakosoana na tutaelekezena na hatimaye tutachagua mmoja awe miongini mwetu kuwa kiongozi wa Wabunge watano. Ni matumaini yangu kwamba uchaguzi huu umemalizika vizuri umejenga umoja miongoni mwetu wana CCM na hili ni jambo ambalo tumelizowea wana CCM, chaguzi kila mara zinafanyika na baada ya uchaguzi mambo yote yanakuwa yamepita.

Mhe. Spika, kwa hivyo nimalizie kwa kuwashukuru sana. Naomba mtuamini kwamba tutawawakilisha vizuri katika Bunge la Jamhuri kwa jambo lolote ambalo lina maslahi ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mhe. Spika, naomba nimalizie hapo nawashukuru tena. (*Makofi*)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika ahsante sana, nichukuwe fursa hii na mimi kuungana na Mhe. Machano Othman Said kuwashukuru wote walionipigia kura na wale waliokuwa hawakubahatika kunipa kura, walionipa kura 16 za hapana, wametumia demokrasia yao, ni haki yao ya msingi wala hawakufanya ubaguzi. Hata Wajumbe tunapokuja humu tunakuwa kumi, kumi na tano tunamchagua mmoja na tukamuamini. Kwa hiyo, nawashukuru kwa dhati, na vidole hivi Mhe. Spika, haviko sawa.

Kwa hiyo, kubwa hapa mimi nashukuru kwa dhati kabisa walionichagua na wasionichaguwa wala sihisi kuwa kutakuwa na kinyongo ni wajibu wao wa demokrasia. (*Makofi*)

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa): Mhe. Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuujaalia uchaguzi huu kwenda salama, kwa nia njema kabisa kuchaguliwa na Wajumbe kura kama hizi nilizozipata nawashukuru sana.

Mhe. Spika, pia nimshukuru kwanza Makamu wa Pili wa Rais kama nilivyosema baba yangu namshukuru sana, namuheshimu, nampenda kwa hivyo namshukuru sana. (*Makofi*)

Pia, niwashukuru sana mawaziri wangu wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuniunga mkono kwa kupata kura nyingi.

Pia, niwashukuru sana Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi ambao ni wengi naahidi mbele yako Mhe. Spika, nitashirikiana nao kwa hali na mali

wajumbe hao wote kwa kunipa kazi hii nzito na kwa kuniamini na kwa kujua kuwa nitaifanya kwa nia njema na nchi yetu. Basi nawashukuru sana na kazi hii nitaifanya na Mwenyezi Mungu naomba anisaidie kwa dhati ili niweze kufanikisha yale malengo ya wajumbe hawa waliyokuwa wanayataka.

Vile vile niwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Mtoni kwa kunichaguwa pia kufika hapa kwenye Baraza lako hili tukufu Mhe. Spika. Kwa hiyo, na wao nawashukuru sana. Baada ya kusema hayo shukurani zangu naomba sana kuwashukuru tena Wajumbe wote wa Baraza hili tukufu kwa kunichagua kwa kura nyingi sana 63. Mimi nasema ahsanteni imani kubwa mmenionesha na mimi nitakulipeni imani yenu hiyo. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii na mimi niungane na wenzangu kuwashukuru wajumbe wote ambao wametupigia kura na naomba niwashukuru sana kwa kunipigia kura za ndio 70 na zile tatu ambazo zimekataa Mhe. Spika, wametumia demokrasia yao. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kama wajumbe walivyoniamini naomba na mimi nizidi kuwasisistiza kwamba waniamini, nitaliwakilisha Baraza hili na Zanzibar kwa ujumla katika Bunge la Jamhuri ya Muungano na kwamba sitawaangusha. (*Makofi*)

Mhe. Spika, lakini uwakilishi wangu utakuwa imara zaidi pale wajumbe watakapoonesha mashirikiano kwa kuniongoza, kunishauri na kunipa mambo yote yale ambayo wanahisi labda ningeweza kuyawakilisha katika Bunge la Jamhuri.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo niwashukuru tena wajumbe kwa kura zao za ndio ambazo walinipa. (*Makofi*)

Mhe. Amina Idd Mabrouk: Mhe. Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuweza kusimama tena mbele ya Baraza lako tukufu nikiwa na nguvu na afya njema. (*Makofi*)

Pia, nichukue nafasi hii ya dhati kabisa kukushuru wewe Mhe. Spika, kwa kuongoza uchaguzi huu kuwa wa huru na wa haki. (*Makofi*)

Mhe. Spika, pia nichukuwe nafasi hii ya dhati kabisa kuwashukuru Waheshiwa Wajumbe Wawakilishi wote wa Baraza hili la Wawakilishi kwa kunichagua mimi kuwawakilisha katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, sitakuwa na maneno mengi zaidi ili nisiwachoshe lakini niahidi kwamba, kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu basi niseme kuwa kura zao walizonipigia kwa wingi za ndio basi niwahakikishie kwamba hawatojuta kunipa kura zao. (*Makofi*)

Pia.,niahidi kwamba, kwa kushirikiana sisi sote watano basi tutawawakilisha vyema katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini kwa kushirikiana na wao Waheshimiwa Wawakilishi, ewe Mwenyezi Mungu nisaidie. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Amina Idd Mabrouk na hapo ndio tutakuwa tumefikia mwisho wa shughuli zinazohusu uchaguzi. Katibu kama kuna shughuli nyengine inayoendelea.

Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa shughuli zote ambazo zimepangwa katika *order paper* ya leo zitakuwa zimekamilika, naomba kabla sijaakhirisha sasa nitoe matangazo mawili.

Kwanza mnatangaziwa na Mhe. Machamo Othman Said Mwenyekiti, anaitangazia kamati yake Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Bora wakutane mara baada ya kuakhirishwa kwa kikao hiki.

Tangazo jengine ni la Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake wanajuilishwa kuwa kile kikao chao na Jumuiya ya Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu na chenyewe kitafanyika mara baada ya kusitishwa kwa shughuli zetu wakati huu katika ukumbi wa juu wa mikutano. Tangazo hili limeletwa na Katibu wa Kamati.

Baada ya hapo napenda niakhirishe shughuli za Baraza mpaka kesho siku ya Ijumaa, tarehe 27 saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa. 6:18 mchana Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 27/06/2016 saa 3.00 asubuhi)